

**Mwinyi** ashukuru Saudi Arabia kwa misaada maendeleo

UK. 3



**Mabalozi** waanza safari kupanda kilele Kilimanjaro

UKURASA 4



UK. 22


# Nipashe

Jumamosi Desemba 9, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581519

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ

0745 700710 LIKE & FOLLOW US


## SUAREZ MCHEZAJI BORA LIGI KUU YA BRAZIL



# Ni vilio nauli mpya mabasi

UKURASA 2

UKURASA WA 8

**MIAKA 62 UHURU:**

## Kutoka Nyerere Ujamaa hadi Kazi Iendelee

## Mvua yageuka fursa madereva wa bajaji, bodaboda

UKURASA 3



Askari wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), wakiendelea kufanya usafi kwa kuondoa tope kwenye mji mdogo wa Katesh, wilayani Hanang' mkoani Manyara jana. **PICHA: GIFT THADEY**

MAAFA KATESH

UKURASA 4

# Vifo vyafikia 86, majeruhi waongezeka


**MICHEZO** **SIMBA, WYDAD MECHI YA HESABU** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Mkuu wa Kitengo cha Utafiti cha Jeshi la Polisi nchini, ACP Ralph Meela akitoa elimu kuhusu ukatili wa kijinsia kwa mamalishe na wauza matunda wa soko wakulima la Sterio, Temeke Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia yaliyofadhiliwa na kampuni ya Barrick. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vilio kila kona nauli mpya mabasi

**Na Waandishi Wetu**

NAULI mpya zilizoanza kutumika jana zimesababisha vilio kwa wananchi katika mikoa mbalimbali huku baadhi ya abiria wakizigomea na wengine kutembea kwa miguu.

Baadhi ya abiria waliozungumza na Nipashe jana waliitupia lawama Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kuwa haijawashirikisha na ongezeko hilo huku wakilitafsiri kuwa ni maumivu kwao kwa kuwa halijazingatia hali ya uchumi wa mtu mmoja mmoja.

Mkazi wa Njombe Mjini, Erasto Mhagama, alisema hawafahamu mamlaka imezingatia vigezo gani hadi kupandisha nauli hizo ilhali hali ya uchumi wa mtu mmoja mmoja kwa sasa ni ngumu.

"Hawa watu wa usafirishaji walisema wamefanya mjadala na kujadiliana na abiria, wananchi wakakubaliana, hivi ni wananchi gani hao waliofikiwa?. Hizi nauli mpya ni kubwa sana hii si sawa.

"Kwa mfano, Njombe-Dar es Salaam kwa mara ya mwisho mimi nimekata tiketi kwenye moja ya basi hapa mjini ilikuwa Sh. 42,000 sasa ni Sh. 48,000, unajiuliza ongezeko hili linatokana na bei za mafuta au ni nini? Mafuta yameshuka lakini nauli zimepanda mara dufu," alisema.

Gaudio Tweve, ameitaka serikali wanapofanya mabadiliko kama hayo ni vyema utekelezaji wake ukawa kwa mwaka wa fedha unaofuata.

"Unatangazeje kupanda kwa nauli Desemba 8, mwaka huu, ndo msimu ambao wanafunzi waliokuwa shuleni wanarejea nyumbani na wazazi tulidunduliza fedha kwa ajili ya nauli zao halafu mnatutangazia ongezeko jipya. Hii si sawa," alisema Tweve.

Deo Mwinuka alitofautiana na abiria wengine akisema kuwa, nauli zilizotangazwa na LATRA ni sahihi kwa kuwa, zimetolewa kwa kuangalia kilometa.

"Ninachoweza kusema ni kwamba waangalie utaratibu wa kutangaza usiwe wa kushtukiza ili kumpa muda mwananchi kujua nini kinafuata na kupanga bajeti zake," alisema Mwinuka.

**WALANGUA NAULI**

Mkoani Singida, wakatishaji wa tiketi wametumia fursa ya ongezeko hilo kupandisha zaidi nauli kulinganisha na zile zilizotangazwa na LATRA.

Baadhi ya abiria jana walikutwa katika kituo kikuu cha mabasi cha Misuna, mjini Singida akiwamo mwanafunzi Shule ya Sekondari ya Dk. Olsen, Happiness Wanjala na Hellen Innocent, wakilalamikia kuwapo kwa bei tofauti za nauli kwa abiria.

Happiness na Hellen walisema wao wamelipa Sh. 30,000 kwa safari ya Singida hadi Mwanza badala ya Sh. 27,000 kwa safari hiyo hiyo wakati Nanah Godfrey amelipa Sh. 31,000. Wananchi katika mikoa ya Kanda ya Ziwa, wamepinga ongezeko hilo wakieleza kuwa serikali haijawatendea haki kwa kupandisha nauli bila kujali gharama za maisha zilivyopanda mara dufu.

Farida Hussein, mfanyabiashara mdogo wa genge la nyanya na mboga katika eneo la Malimbe mkoani Mwanza, alisema kila siku amekuwa akienda katika mwalo wa dagaa wa Mswahili kufuata dagaa wabichi, lakini ongezeko la nauli kwake litaathiri biashara yake kwa kuwa badala ya kulipa Sh. 500 ya awali, sasa analazimika kulipa Sh. 1,000.

Abiria Enelietha Robert alisema ameshindwa kusafiri na familia yake jana kutoka Bukoba kwenda Mwanza, baada ya kufika kituoni na kukutana na mabadiliko ya nauli.

Mkazi wa Shinyanga, Elbariki Deogratius, aliiomba serikali kuangalia upya suala hilo kwa sababu badala ya kuwapunguzia makali ya maisha, sasa limeyaongeza huku hali ya uchumi kwa mtu mmoja mmoja ikiwa si nzuri.

**MAWAKALA WALIA**

Wakala wa kampuni moja ya mabasi katika kituo cha mabasi yaendayo mikoani Nyamohongolo, Hassan Mwalijo, alisema ongezeko hilo limesababisha kuwapo kwa mwitikio mdogo wa abiria kusafiri.

Alisema nauli ya Mwanza-Moshi imeongezeka kwa Sh. 7,000 wakati awali ilikuwa Sh.45,000 na sasa imefikia Sh.52,000.

Wakala wa Usafiri katika Stendi ya Mabasi Soko Kuu Manispaa ya Shinyanga, Seleman Hamad, alisema kutokana na abiria wengi kugomea nauli mpya, wamelazimika kuendelea na iliyokuwapo kwa abiria wanaotoka Shinyanga Mjini hadi Kahama.

Kondakta wa kituo cha abiria Nata mkoani Mwanza, Mussa Kiboma, aliiomba serikali kutoa elimu kuhusu ongezeko hilo ili kuondoa migogoro inayojitokeza baada ya utekelezaji wa nauli mpya kuanza. James Wilson ambaye ni kondakta wa gari linalofanya safari kati ya Karagwe na Bukoba mjini, mkoani Kagera, alisema kukosekana kwa elimu kumewachonganisha na abiria ambao wamegoma kulipa nauli mpya.

"Leo (jana) kama unavyoona gari halijajaa na si kawaida. Tunatoka kituoni na abiria wachache, hatufahamu ni kutokana na kupanda kwa nauli au la. Hata wanaofika kituoni ukiwaambia ongezeko wanalalamika. Serikali itatue tatizo hili," alisema.

Mmiliki wa mabasi yaendayo mikoani kutoka katika kituo cha mabasi cha Nyegezi, Joseph Pauline, alisema walipokea ongezeko la nauli kama neema kwao, lakini katika utekelezaji wake wanakumbana na idadi ndogo ya abiria.

Pauline aliiomba serikali kuangalia utaratibu mbadala ikiwa ni pamoja na kushusha bei za mafuta ili wananchi wenye kipato cha chini wasiathiriwe na ongezeko la nauli.

**DODOMA WATEMBEA**

Baadhi ya abiria jijini Dodoma jana walisusa kupanda daladala na kuamua kutembea baada ya nauli iliyokuwa Sh. 500 kupanda hadi Sh. 600 na waliyokuwa wakilipa Sh. 900 sasa imefikia Sh. 1,000.

Dereva Kassim Timamu, anayefanya safari zake stendi ya Machinga Complex hadi Swaswa alisema, amelazimika kutoa elimu ya kupanda kwa nauli kwa kuwasomea abiria tangazo lililotolewa na LATRA ambalo linaonyesha viwango vipya vya nauli za daladala.

**DAR, ARUSHA MOTO**

Mkazi wa Tandika, Dar es Salaam, Said Yassin, alisema, "Mimi nilitoka nyumbani na 1,000 ambayo ni nauli ya kuja Kariakoo na kurudi nyumbani, lakini nikarudishiwa Sh. 400, abiria tulikuja juu tukataka turejeshewe Sh. 100 zetu." alisema.

Kondakta wa daladala la Tegeta-Kariakoo, Mwinyi Haji, alisema wamekuwa katika wakati mgumu kutokana na abiria kudai hawafahamu kama kuna ongezeko la nauli, hivyo baadhi kutoa nauli kamili ya zamani."

Jackline Masawe Mkazi wa Msasani Kata ya Murieti jijini Arusha, alisema suala la upandaji nauli limemsikitisha na limesababisha vurugu kwenye magari kwa sababu walio wengi walikuwa hawana ufahamu huo.

LATRA ilitangaza nauli mpya Novemba 27, mwaka huu, na kuelekeza hadi kufikia jana (Desemba 8) zitaanza kutumika ambapo jana ilitangaza kuwa, hakuna pingamizi lolote walilopokea kutoka kwa wadau tangu watangaze nauli hizo. Mamlaka hiyo ilitangaza ongezeko la nauli baada ya kupitia maoni ya wadau na kutoa siku 14 kwa watu kuwasilisha pingamizi kuhusu nauli mpya.

## MAAFA KATESH
## Vifo sasa vyafikia 86, majeruhi waongezeka

**Na Waandishi Wetu**

SERIKALI imesema idadi ya vifo vilivyotokana na mafuriko na maporomoko ya tope katika mji mdogo wa Katesh, wilayani Hanang, mkoani Manyara, vimefikia 80.

Aidha, majeruhi katika tukio hilo hadi jana walikuwa ni 133 na waathirika wanaohudumiwa katika kambi mbalimbali wakiwa ni 440.

Msemaji Mkuu wa Serikali, Mobhare Matinyi, alitoa taarifa hiyo jana kwa waandishi wa habari akisema kati yao, watu wazima ni 48, wanaume 19 na wanawake 29, watoto 32 wa kike wakiwa ni 17.

"Mwili wa mtoto wa kiume ambao awali ulikuwa haujatambuliwa, umeshatambuliwa. Kuna mwili wa mwanamke mtu mzima umepatikana leo (jana) ambao haujatambuliwa. Jumla ya miili iliyotambuliwa mpaka sasa ni 79," alisema.

Matinyi alisema hadi mchana wa jana majeruhi waliopokelewa katika hospitali walikuwa ni 133 kati yao watu wazima ni 71, wanaume wakiwa ni 33 na wanawake ni 38, watoto ni 62 kati yao wakiume wapo 28 na wa kike ni 34.

"Itakumbukwa siku ya kwanza walipokea majeruhi 117 baada ya wengine kuruhusiwa kurejea nyumbani,"alisema Matinyi na kuongeza kuwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Manyara, kuna watu 18, Hospitali ya Wilaya ya Tumaini 26 na Kituo cha Afya Gendabi wako saba.

Alisema waliopo kwenye kambi mbalimbali ni 440, katika Shule ya Sekondari Katesh wapo 244, Shule ya Msingi Gendabi 168 na Shule ya Msingi Ganana idadi yao ni 28.

Matinyi alisema serikali haitarajii kuweka kambi hizo kwa muda mrefu badala yake itafanya juhudi au kuwarejesha waathirika kwenye jamii au kuwasaidia kuanza makazi mapya baada ya tathmini kukamilika.

Pia alisema serikali imefanya uchunguzi wa kitaalam kwa kutumia vipimo vya ramani uliowezesha kuchora ramani sahihi ya eneo lililoathirika baada ya kufanyia ukaguzi wa kutembea kwa miguu. "Kwa kuhusisha na ripoti za sensa ya Agosti, 2022, ambazo zilikuwa zikitambua pia, vipimo vya ramani kwa kila nyumba, serikali inatarajia itapata ukubwa wa eneo na idadi ya nyumba," alisema.

Matinyi alisema hatua inayofuata ni kufahamu idadi ya kaya na watu waliokuwa wakazi katika nyumba hizo kama kulitokea ongezeko lolote la nyumba na kaya au watu.

"Kazi hii itahusisha wataalamu wa anwani za makazi na vilevile serikali za mitaa na hatimaye tutapata picha kamili ya idadi ya nyumba, kaya na watu walioathirika kwa maana ya kupoteza maisha, kujeruhiwa, walipoteza makazi au uharibifu kwenye makazi," alisema.

Pia alisema itaangaliwa ukubwa wa mashamba ya wananchi yaliyosombwa na mafuriko hayo.




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Jenista Mhagama (kulia), akipokea msaada wa vitu mbalimbali vikiwemo vyakula kwa ajili ya kusaidia wahanga wa mafuriko Kateshi kutoka kwa Meneja Mauzo wa kampuni inayozalisha vinywaji ya Bonite Bottlers mkoani Manyara, Thadeus Massawe (wa pili kulia) jana. Kushoto ni Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel. **PICHA: JALIWASON JASSON**

# Mvua zageuka fursa madereva bodaboda

**Na Waandishi Wetu**

MVUA zinazoendelea kunyesha nchini zimeleta fursa kwa vyombo vya moto na maumivu kwa abiria baada ya bodaboda na bajaji kupandisha nauli maradufu kutokana na baadhi ya barabara kufungwa ikiwamo ya Jangwani, Dar es Salaam.

Baada ya baadhi ya barabara kujaa maji jana jijini Dar es Salaam, madereva wa vyombo hivyo walitumia fursa hiyo kubeba abiria waliokuwa wakishuka kwenye daladala na mwendokasi kwa kuwatoza Sh. 10,000 kwa safari badala ya Sh. 5,000.

Nipashe ilishuhudia mabasi ya mwendokasi yaliyokuwa yakielekea katikati ya mji yakishusha abiria maeneo ya Magomeni Mapipa baada ya mafuriko kutokea barabara ya Jangwani na kusababisha kufungwa kwa muda.

Kutokana na kadhia hiyo, baadhi ya abiria walisema wamelazimika kuchukua usafiri mwingine kwa gharama kubwa ili kuwahi kwenye biashara na ofisini.

Abiria Angel Masawe, alisema bajaji kutoka Msimbazi hadi Mbezi wamewatoza Sh. 7,000 wakati nauli huwa Sh. 3,000.

Alisema kwa usafiri wa bodaboda kwa njia ya Ubungo kwenda Kariakoo, mtu mmoja ni Sh. 10,000 badala ya Sh. 5,000.

"Usafiri wa leo (jana) ni wa hekaheka ndugu zangu wamepata shida sehemu ya kulipa Sh. 3,000 kwa usafiri wa bajaji tumelipa Sh. 7,000 na kwa mvua hii hakuna namna. Utake usitake utalipa maana tunaotumia barabara ya Jangwani tumefika hapa Magomeni tumeshushwa kwenye mwendokasi kwa sababu barabara imefungwa," alisema.

Adinani Ally, alisema alitoka Magomeni saa mbili asubuhi na kufika Kariakoo saa tano baada ya kupita njia ya Kigogo ambayo ndiyo magari mengi yalielekea huko baada ya Jangwani kufungwa.

Maeneo mengine Dar es Salaam yaliyokumbwa na tatizo ni Mwananchi baada ya maji kujaa katika daraja na kusababisha magari yaliyokuwa yakitokea Tabata Kisiwani kwenda barabara ya Mandela kushindwa kupita.

Kutokana na kadhia hiyo, baadhi ya magari yalilazimika kubadili uelekeo hadi Tabata Mawenzi ili kufika mjini au maeneo mengine waliyokuwa wakielekea wakati huo.

Maeneo mengine ambayo barabara zilisababisha shida ni Sinza Makaburini, Keko Furniture ambako maji yalijaa na kusababisha foleni ya magari kwa muda mrefu.

Khadija Yusuph mfanyabiashara katika soko la Kariakoo, alisema mvua hizo zimewaletea athari kutokana na watu kushinda sokoni hapo kwa ajili ya mahitaji yao hasa katika msimu huu wa sikukuu.

"Unakaa dukani muda mrefu huoni wateja, lakini changamoto nyingine ni chemba za maji taka, mvua kama hizi zikinyesha zinamwaga maji barabarani na hii ni hatari kwa afya zetu kwa sababu kuna wanaouza vyakula humu," alisema.

**KILIMANJARO**

Mkoani Kilimanjaro, wakazi wa Kata za Bangalala, Vudee, Chome na Makanya katika Wilaya ya Same, wamejikuta hawana mawasiliano ya barabara, baada ya daraja la Kiengero kukatika kutokana na mafuriko ya mvua zilizonyesha usiku wa Desemba 7, mwaka huu.

Baadhi ya wakazi wa vijiji hivyo, wakiwamo Sebastian Mndeme na Ashura Mzava, kwa nyakati tofauti walisema kukosekana kwa mawasiliano hayo, kumewasababishia adha kubwa ya usafiri.

Meneja wa TANRODS, Mkoa wa Kilimanjaro, Motta Kyando, akizungumza na mwandishi wa habari hizi alisema,"Ni kweli daraja limekatika na mimi nimeshakwenda katika eneo hilo na kujionea uharibifu huo uliotokana na mvua zinazoendelea kunyesha.

"TANROADS tunapambana usiku na mchana, kuhakikisha tunatatua tatizo hilo ndani ya muda mfupi. Nia yetu ni kuhakikisha tunarejesha huduma hiyo ya mawasiliano ya barabara kwa wananchi wa kata hizo," alisema.

Daraja hilo, ndilo linalounganisha pia barabara inayokwenda kwenye masoko ya Mwembe ,Same na Mgagao.

**Imeandikwa na Anjela Mhando na Mary Mosha (MOSHI) na Beatrice Shayo (DAR)**

# Mwinyi ashukuru Saudia misaada ya kimaendeleo

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameishukuru Saudi Arabia kwa jitihada kubwa inazozifanya kwa Tanzania katika kuunga mkono miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo afya, maji, miundombinu ya barabara na uzalishaji umeme.

Aliyasema hayo jana Ikulu, Zanzibar alipozungumza na Balozi wa Saudi Arabia nchini Tanzania, Yahya Ahmed Okeish, aliyefika kujitambulisha. Alisema kuwapo kwa ubalozi huo nchini ni mwendelezo wa ushirikiano mwema uliopo baina ya Tanzania, ikiwamo Zanzibar na Saudi Arabia.

Dk. Mwinyi aliishukuru serikali ya Saudi Arabia kwa kuisaidia Tanzania katika uzalishaji wa umeme, kuunga mkono ujenzi wa barabara ya Wete, Pemba pamoja na kusaidia ukarabati mkubwa wa Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja, Unguja.

Hospitali hiyo inatarajiwa kufanya upasuaji mkubwa zaidi baada ya kumalizika kwa ukarabati wa vyumba vya upasuaji vinavyotarajiwa kuwa na vifaa vya kisasa kwa msaada wa Mfuko wa Saudia.

Rais Dk. Mwinyi pia aliikaribisha Saudi Arabia kuwekeza kwenye Shamba la Makurunge, Bagamoyo, linalomilikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambalo linafaa kwa uwekezaji wa kilimo, uvuvi na utalii. Dk. Mwinyi aliendelea kuishukuru Saudi Arabia kwa msaada mkubwa kwa Zanzibar kupitia sekta ya afya kwa kutoa timu ya madaktari wa upasuaji iliyojitolea kuweka kambi na kuwatibu Wazanzibari.

Aidha, alipongeza timu ya madaktari 21 kutoka Saudi Arabia waliojitolea kuweka kambi ya matibabu kwenye jimbo la Gando kisiwani Pemba ambako waligundua zaidi ya kesi 680 na kufanya upasuaji.

Alisema kambi za matibabu ni moja ya eneo muhimu la ushirikiano uliopo baina ya Zanzibar na Saudi Arabia kwa kuwa zimekuwa na msaada mkubwa kupunguza changomoto nyingi kwenye sekta ya afya nchini.

Mbali na afya, Dk. Mwinyi aligusia maeneo mengine ya ushirikiano yakiwemo uwekezaji, biashara, uvuvi na kilimo cha samaki kupitia sekta ya uchumi wa buluu.

"Tunahitaji uwekezaji zaidi, hasa kwenye Uchumi wa Buluu. Nchi yetu imezungukwa na bahari, sera yetu kuu ya uchumi ni 'Uchumi wa Buluu', hivyo tunahitaji uwekezaji mkubwa kwenye eneo hilo, kupitia uvuvi na kilimo cha Samaki," alisema.

Katika hatua nyingine, Rais Dk. Mwinyi aliipongeza Saudi Arabia kwa kuchaguliwa kuwa mwenyeji wa maonyesho makubwa ya biashara duniani, (Expo 2023).

Balozi Yahya alisema Saudi Arabia imekuwa na msaada mkubwa kwa Afrika ikiwamo Tanzania na Zanzibar pia itanufaika kwa kiasi kikubwa na fursa nyingi baada ya kutiwa saini kwa makubaliano ya mamilioni ya dola za Marekani zilizoelekezwa Afrika.

Alisema Tanzania na Saudi Arabia kwa muda mrefu, zimekua zikibadilishana uzoefu baina yao kupitia sekta mbalimbali za ushirikiano wao.

Balozi Yahya pia aliambatana na timu ya madaktari wa upasuaji 21 kutoka Saudi Arabia ambao walikuwapo kisiwani Pemba kwenye jimbo la Gando walikoweka kambi ya matibabu kwa maradhi mbalimbali.

Kiongozi wa timu ya madaktari hao, Dk. Aiman Al Soluman, alisema waligundua kesi 689 kati ya wagonjwa wengi waliojitokeza kwenye kambi ya matibabu, kati ya hizo, 303 zilifanyiwa upasuaji.

Alisema wagonjwa wa upasuaji wa jumla walikuwa 124 kati yao 76 walifanyiwa upasuaji wa jumla. Pia alisema waligundua matatizo ya mfumo wa mkojo kwa watoto na watu wazima kwa kesi 112 na kesi 78 zilifanyiwa upasuaji.

# Mabalozi wapanda Mlima Kilimanjaro

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

UJUMBE wa mabalozi 11 wanaoiwakilisha Tanzania katika mataifa mbalimbali duniani, wameanza safari ya siku saba ya kupanda Mlima Kilimanjaro kwa ajili ya kuongeza motisha kwa wazalendo 228 wanaopeleka bendera ya taifa katika kilele cha Uhuru.

Mabalozi hao ni wale walioko katika nchi za Cuba, Ufaransa, Malaysia, Ubelgiji, Umoja wa Ulaya (EU), Riadh-Saudi Arabia, Australia, New Zealand, Brazil na Japan.

Akizungumzia safari hiyo inayoratibiwa chini ya Kampeni ya Twenzetu Kileleni 2023, Ofisa Mahusiano wa Kampuni ya Utalii ya ZARA Tours, Ibrahim Juma, alisema katika ujumbe huo, wamo askari na maofisa wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ).

Alisema maofisa wengine ni taasisi za serikali, ambao wameungana kuchagiza Maadhimisho ya Miaka 62 ya Uhuru, yatakayofanyika leo nchini.

Aliwataja mabalozi hao kuwa ni Humphrey Polepole (Cuba), Dk. Mahadhi Juma Maalim (Malaysia), Jestas Nyamanga (Ubelgiji, EU), Dk. Molid Juma Abdallah (Riadh-Saudi Arabia), Alli Jabir Mwadini (Ufaransa) na Baraka Luvanda (Australia, New Zealand).

Wazalendo hao wanapanda mlima huo kwa kutumia malango matatu tofauti ya Lemosho (Siha), Machame (Hai) na Marangu (Moshi).

Kabla ya kuanza safari hiyo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), Jenerali Mstaafu, George Waitara, aliwataka mabalozi hao kuendelea kutangaza utalii na kuvutia wawekezaji nchini hasa katika maeneo ya miundombinu, usafirishaji na hoteli za kisasa.

"Tanzania kuna vivutio vingi sana na bado tuna maeneo ya uwekezaji, mabalozi mnaoshiriki kampeni hii, ongezeni nguvu katika kutangaza maeneo ya uwekezaji.

"Kazi mojawapo ya mabalozi, ni kutangaza utalii. Hivyo, nafasi hii ya kupanda mlima kwa mabalozi wetu, itasaidia kuutangaza mlima kwa kuwa mtakuwa mmeutambua vyema na mtaweza kuelezea popote."

Kiongozi wa ujumbe wa mabalozi hao, Dk. Maalim, alisema ziara yao hiyo itawasaidia kuelewa vizuri mlima huo ili watakapokuwa wakiutangaza nje ya Tanzania waelezee uhalisia wake. Awali, Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Kisare Makori, alisema mlima huo umebeba historia kubwa ya Uhuru wa Tanganyika, lakini kwa sasa unakabiliwa na uvamizi wa mifugo katika eneo la hifadhi, ukataji miti, ujangili na uwashaji moto hovyo.

Kiongozi wa askari na maofisa wa JWTZ, Kanali Martin Msumari, alisema wanatarajia kusimika bendera hiyo Disemba 9, mwaka huu katika kilele hicho chenye urefu wa mita 5,895 kutoka usawa wa bahari.

## Uchafuzi mazingira chanzo uchumi kudorora

**Na Jenifer Gilla**

MKUU wa Idara ya Mazingira Kitengo cha Taka Ngumu na Usafishaji wa Manispaa ya Temeke, Mkana Mohamed, amesema uchafuzi wa mazingira hurudisha maendeleo nyuma kwa kuwa fedha za kujenga uchumi hutumika kutibu maradhi.

Alisema zaidi ya asilimia 70 ya magonjwa hutokana na uchafu, hivyo ukidhibitiwa utatokomeza maradhi ya mara kwa mara na fedha hizo zikaelekezwa kujenga uchumi.

Aliyasema hayo juzi katika hafla ya kukabidhi mradi wa taka sifuri kwa Shule ya Sekondari ya Kibasila uliotolewa na Taasisi ya Mazingira Plus kwa kushirikiana na TCCI Mazingira, Dar es Salaam.

Mradi huo unahusisha kizimba cha kutenganisha na kupembua taka pamoja na kuwajengea uwezo wanafunzi namna ya kubadilisha taka hizo kuwa fursa ya kiuchumi.

Alisema mtu anapougua magonjwa hayo kama vile kipindupindu anachukua muda mwingi kujiuguza na wengine hufariki hali inayoipunguzia taifa nguvu kazi katika kujenga uchumi.

Alisema mradi wa taka sifuri ni mfano wa kuigwa na jamii kwa kuwa lengo lake ni kuhakikisha hazipelekwi dampo bali zinatafutiwa shughuli nyingine na kuipa jamii fursa ya kujiingizia kipato.

Alisema shule hiyo haikuchaguliwa kwa bahati mbaya kuwa mwanzilishi wa mradi huo nchini, bali ni miongoni mwa zinazofanya vizuri katika masomo, hivyo wanafunzi waliojengewa uwezo watakuwa walimu kwa shule nyingine. "Tunaona kuwa taka za plastiki, vyuma vinahitajika viwandani kutengenezea malighafi nyingine na hata hizi taka za majumbani zinahitajika viwandani na majumbani kutengenezea mbolea ya chakula," alisema.

Mratibu wa mradi huo kutoka Mazingira Plus, Ramadhani Mwakae, alisema wamewajengea uwezo wanafunzi namna ya kubadilisha taka kuwa fursa za kiuchumi.

Alisema lengo la mradi huo ni kuunga mkono juhudi za serikali kuhakikisha asilima 80 ya taka ngumu zinazozalishwa hazitupwi jalalani kwa kuweka miradi hiyo mashuleni ili kuandaa vizazi vijavyo vyenye utamaduni wa kutunza mazingira.

Mkuu wa Shule hiyo, Patrick Sinyinza, alisema amesikia faraja kuwa mwanzilishi wa mradi huo muhimu katika uhifadhi wa mazingira nchini na kuwa watafanya bidii ili wawe mfano wa kuigwa.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya BUGANDO Wilaya ya GEITA**
**Mkoa wa GEITA**
**Shauri la MADAI Na 98/2023**
**Jina la Mdai: UMOJA WA WAFANYA BIASHARA NKOME**
**Jina la Mdaiwa: MOSHI ELIAS**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuniya 18 ya kanun iza taratibu Madai katika mahakama za Mwanzo)**

**Kwa:MOSHI ELIAS WA NKOME**
AMRI: - Unaamriwa na Jamuhuri uhudhurie Mahakamani hapa siku ya Jumanne tarehe 23/11/2023 saa 2:00 Asubuhi ili ujibu madai ya Fedha Tsh.639,000/-. Usipohudhuria kesi itasikilizwa bila wewe kuwepo Unaonywa usikose kuhudhuria.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo Tarehe 20 Mwezi 11 Mwaka 2023

**HAKIMU**



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**YA WILAYA YA MOROGORO**
**KITUO CHA MJINI**
**MKOA WA MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na……130/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: HAMISI ALLY SUKU wa ANANASIFU**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOTOLEWA NA SAID HAMISI SUKU**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 13 Mwezi 12 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;
- Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia

Imetolewa leo tarehe 6 mwezi 12 mwaka 2023
……………………………………
**HAKIMU**



**KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA**



SAMSON GADIEL MACHA ANATANGAZA KUPOTELEWA NA HATI YA KUSAFIRIA "PASSPORT" YENYE USAJILI NAMBA TAE481962 YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI TAARIFA NAMBA PHQ/IRI/IRI/3968/2023.



**ARM SOLUTION AUCTION MART AND PROPERTY MANAGEMENT CO LTD**

**MNADA WA HADHARA**

KWA IDHINI TULIYOPEWA NA **MuCoBa Bank Plc** TUNAWATANGAZIA WANANCHI WOTE KUWA KUANZIA **TAREHE 21-12-2023** NA KUENDELEA TUTAUZA KWA MNADA WA HADHARA MALI ZA WADAIWA HAPO CHINI ILI KUFIDIA MADENI WANAYODAIWA

| S/N | JINA LA MDAIWA | JINA LA MDHAMINI | TAWI ALILOKOPA | DHAMANA | MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | JOEL KIBELENGE LUGANGILA | JOEL KIBELENGE LUGANGILA | MAFINGA | SHAMBA NA MABWAWA YA KUFUGIA SAMAKI NA NYUMBA | MAFINGA SAO HILL | Kuanzia saa 3 asubuhi |
| 2 | ALEXANDER JOHN SEYARI | ALEXANDER JOHN SEYARI | MAFINGA | PAGALE | MAFINGA - BOMA | Kuanzia saa 3 asubuhi |
| 3 | ABDALAH MSAFIRI NZINGO | MSAFIRI NZINGO | MAFINGA | NYUMBA | MAFINGA - CHANGARAWE | Kuanzia saa 3 asubuhi |
| 4 | AMOS SANGA | AMOS SANGA | ILULA | NYUMBA | IRINGA - ILULA | Kuanzia saa 3 asubuhi |
| 5 | METHEW NALOLE | METHEW NALOLE | MAFINGA | PAGALE | MAFINGA - CHANGARAWE | Kuanzia saa 3 asubuhi |
| 6 | JOEL PETER MAKOLO | JOEL PETER MAKOLO | MADIBILA | NYUMBA | MADIBILA | Kuanzia saa 3 asubuhi |
| 7 | LUSANI LUTEGO | VASCO KIVEMBELE | MAFINGA | NYUMBA NA SHAMBA | NYOLOLO - IHANGANATWA | Kuanzia saa 3 asubuhi |
| 8 | EDSON KILAMLYA | EDSON KILAMLYA | IRINGA | NYUMBA | IRINGA - IPOGOLO | Kuanzia saa 3 asubuhi |
| 9 | REUBEN MWAKASALA | REUBEN MWAKASALA | MAFINGA | NYUMBA | MAFINGA - IHONGOLE | Kuanzia saa 3 asubuhi |
| 10 | CYNITHIA MTUI | KIGUNGA MWANGWA | IRINGA | KIWANJA | RINGA - MTWIVILA B | Kuanzia saa 3 asubuhi |
| 11 | BONIFACE CHUMO | BONIFACE CHUMO | MAFINGA | NYUMBA | MAFINGA - GANGILONGA | Kuanzia saa 3 asubuhi |
| 12 | GAI GAMBA | GAI GAMBA | MAFINGA | NYUMBA | MAFINGA - CHANGARAWE | Kuanzia saa 3 asubuhi |
| 13 | CHARLES MASHITA | CHARLES MASHITA | MAFINGA | NYUMBA | MAFINGA - IHONGOLE | Kuanzia saa 3 asubuhi |
| 14 | EMMANUEL E. WISSO | EMMANUEL E. WISSO | MAFINGA | NYUMBA | MAFINGA - MGODI | Kuanzia saa 3 asubuhi |
| 15 | GASTON RUGUGA NTAMAKILILO | GASTON RUGUGA NTAMAKILILO | MAFINGA | NYUMBA | MAFINGA - RUNGEMA | Kuanzia saa 3 asubuhi |
| 16 | DICKSON MASASI | DICKSON MASASI | MAFINGA | KIWANJA | MAFINGA - CHANGARAWE MAKALALA | Kuanzia saa 3 asubuhi |
| 17 | STEWART MAGILI | STEWART MAGILI | MAFINGA | NYUMBA | MUFINDI - SAWALA | Kuanzia saa 3 asubuhi |
| 18 | MARRY NGELULA | MARRY NGELULA | MAFINGA | NYUMBA | MAFINGA | Kuanzia saa 3 asubuhi |
| 19 | ROBART PAULO KISEO | ROBART PAULO KISEO | IRINGA | NYUMBA | IRINGA - PAWAGA | Kuanzia saa 3 asubuhi |
| 20 | ANJELO ANDREAS NYEMBEKE | ANJELO ANDREAS NYEMBEKE | MAFINGA | NYUMBA MBILI | MAFINGA - BOMA | Kuanzia saa 3 asubuhi |
| 21 | VAILETH GEORGE HAULE | GREGORY MWINDI | MAFINGA | PAGALE | MAFINGA - RUNGEMBA | Kuanzia saa 3 asubuhi |
| 22 | FABIAN GODFREY YERINDE | JOEL LUGANGILA | MAFINGA | NYUMBA | MAFINGA - IHONGOLE | Kuanzia saa 3 asubuhi |
| 23 | FILBERT YOVENARY KALINGA | FILBERT YOVENARY KALINGA | MAFINGA | NYUMBA | MAFINGA - UPENDO | Kuanzia saa 3 asubuhi |
| 24 | MUSA MAKWETA | MUSA MAKWETA | MAFINGA | NYUMBA | MAFINGA - CHANGARAWE | Kuanzia saa 3 asubuhi |
| 25 | HAJI NYAKWILOLA | HAJI NYAKWILOLA | MAFINGA | NYUMBA | MAFINGA - BOMA | Kuanzia saa 3 asubuhi |
| 26 | ISAYA CUPPUSWAMY | ISAYA CUPPUSWAMY | MAFINGA | NYUMBA | MAFINGA - WAMBI - LUGANGA | Kuanzia saa 3 asubuhi |
| 27 | YUSUPH MKULU | YUSUPH MKULU | MAFINGA | NYUMBA | SADANI - UYELA | Kuanzia saa 3 asubuhi |
| 28 | MUFINDI INSTITUTE OF AGRICULTURE | MUFINDI INSTITUTE OF AGRICULTURE | MAFINGA | SHAMBA LENYE MAPAGALE YA CHUO EKARI 12 | MAFINGA - BOMA - NDOLEZI | Kuanzia saa 3 asubuhi |
| 29 | HENRY IBRAHIM LWEHELA | HENRY IBRAHIM LWEHELA | IGOWOLE | NYUMBA | IGOWOLE | Kuanzia saa 3 asubuhi |
| 30 | MENERICK BEATUS BALAMA | MENERICK BEATUS BALAMA | IRINGA | NYUMBA | IRINGA - KILOLO | Kuanzia saa 3 asubuhi |
| 31 | JOCTAN NYALUKE | JOCTAN NYALUKE | MAFINGA | NYUMBA | MAFINGA - BOMA - KIGAMBONI | Kuanzia saa 3 asubuhi |
| 32 | AZIM HALID MBONAGA | AZIM HALID MBONAGA | MADIBILA | PAGALE | MADIBILA | Kuanzia saa 3 asubuhi |
| 33 | GAUDE NCE CHARLES MOHELE | GAUDE NCE CHARLES MOHELE | MADIBILA | NYUMBA | MADIBILA | Kuanzia saa 3 asubuhi |

# MATANGAZO

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## MAOMBI YA KUONESHA NIA YA KUTOA HUDUMA ZA UFUATILIAJI NA UTOAJI TAARIFA KWA AJILI YA KAMPUNI YA EACOP LTD NCHINI TANZANIA - KUMBUKUMBU NA. 00000438

Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) LTD (''EACOP LTD''), inaalika kampuni zenye uzoefu na weledi wa kutosha kuonesha nia ya kutoa Huduma za Ufuatiliaji na Utoaji Taarifa katika Mradi wa EACOP nchini Tanzania.

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba la kusafirisha Mafuta lililofukiwa chini ya ardhi linalokatisha mipaka ya nchi mbili litakalo safirisha mafuta ghafi Kwenda katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka rasi ya Chongoleani karibu na Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 296 zitakuwa nchini Uganda na kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:**
Kampuni ya EACOP LTD inaalika watoa huduma wenye uzoefu na weledi wa kutosha kuonesha nia yao ya kutoa Huduma zifuatazo za Ufuatiliaji na Utoaji Taarifa nchini Tanzania.

- Kufanya uchambuzi wa kina wa utangazani katika majukwaa mbalimbali, ikiwa ni pamoja na magazeti, mtandao, redio na luninga pamoja na mitandao ya kijamii.
- Kufuatilia na kuchambua shughuli za tasnia ya vyombo vya habari ili kubaini mielekeo ya soko.
- Kutekeleza mifumo ya utambuzi wa mapema wa hali ya hatari inayoweza kutokea na kutoa tahadhari kwa wakati kwa wateja.
- Kuandaa ripoti za kina za kila mwezi na
- Kufuatilia na kuchambua mitandao yote , maoni na ushiriki kwenye majukwaa ya vyombo vya habari vya kijadi.
- Kutoa elimu kuhusu mielekeo na maendeleo ya tasnia ya vyombo vya habari.
- Kutoa huduma ya uwezeshaji wa ufuatiliaji katika mazingira halisi ili kutoa ufahamu wa haraka wa utangazaji wa habari
- Kutumia teknolojia ya hali ya juu na zana bunifu ili kuimarisha usahihi na ufanisi wa michakato ya ufuatiliaji wa vyombo vya habari.
- Kupanua huduma za ufuatiliaji ili kuvifikia vyombo vya habari vya kimataifa.
- Kutoa ripoti za kina kuhusu jinsi utangazaji wa habari unavyoathiiri mtazamo wa umma.
- Kufanya uchambuzi wa hadhira ili kutambua idadi ya watu muhimu na kuweka mikakati ya ufuatiliaji ili kufikia hadhira mahususi kwa ufanisi.
- Kukuza uwezo wa uchambuzi wa kiutambuzi, ili kuweza kufahamu mienendo ya vyombo vya habari na masuala ibuka.

**VIGEZO MUHIMU:**
Makampuni au taasisi zinzoonesha nia zinaalikwa kutuma maombi na kuambatanisha nyaraka zifuatazo:

- Maelezo ya uzoefu, utalaamu na uwezo wa kutoa huduma katika mawanda yanayohitajika
- Wasifu wa Shirika unaoonyesha huduma zinazotolewa, uthibitisho wa utendaji, pampja na barua za utibitisho kutoka kwa wateja watatu wa awali.
- Leseni ya biashara
- Cheti cha usajili toka BRELA (ambatanisha kivuli cha cheti)
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Cheti cha Uthibitisho wa Mlipa Kodi kwa mwaka uliopita.
- Waombaji wanasisitizwa sana kuhakikisha kuwa wamesajiliwa kwenye kanzidata ya EWURA (LSSP) ya Watoa Huduma za Ugavi wa Ndani, wakati wa kuwasilisha maombi ya kuonesha nia,
- Kuzingatia Kanuni za Watoa Huduma wa Ndani za mwaka 2017 na ufafanuzi wa Makampuni ya Ndani
- Wasifu wa wafanyakazi muhimu watakaohusika katika mradi, ikiwa ni pamoja na vyeti vyao vya muhimu, viwango vya elimu, uzoefu , na uwezo wa kutoa huduma zinazohitajika.
- Uwezo wa kifedha wa kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kuwasilisha hesabu za fedha za miaka mitatu iliyopita.
- Uthibitisho kutoka kwenye mfumo wa Usimamizi wa QHSE, taasisi na mchakato kulingana na Viwango vya Ndani na Ki-Sekta vinavyotumika kwa kazi zinayofanana na hii.
- Uthibitisho wa kukubaliana na sera za kupinga rushwa, ufisadi, na Haki za Binandamu

Kampuni zenye nia, ambazo zina uwezo na rasilimali za kutosha kutoa huduma zilizotajwa hapo juu zinapaswa kutuma maombi na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe ya **procurement.tz@eacop.com** (ukubwa wa barua pepe usizidi 20Mb) mnamo au kabla ya **saa 11:00 jioni** kwa saa za Afrika Mashariki (EAT) mnamo au kabla ya tarehe **23 Disemba 2023**. Kichwa cha Barua pepe kiwe **00000438** - Utoaji wa Huduma za Ufuatiliaji na Utoaji Taarifa. Maombi yote yakuonesha nia yawe kati ya kurasa 10 hadi 20.
Maombi yote lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kingereza.

**Muhimu:** Kampuni ya EACOP LTD itapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia kulingana na tangazo hili la kuonesha nia na kufanya tathmini kwa kuzingatia vigezo vya ndani ili kubaini kampuni ambazo zitakazojumuishwa kwenye orodha ya makampuni ya awali yenye vigezo. Mwaliko wa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa makampuni ya awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji waTaarifa (NDA). Kampuni ya EACOP LTD inaheshimu haki katika kufanya maamuzi ya kuchagua au kukataa kampuni na kuheshimu maamuzi yake pasipo kutoa sababu kwa kampuni husika.

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## MAOMBI YA KUONESHA NIA YA UTOAJI HUDUMA YA UCHUKUAJI WA KUMBUKUMBU ZA PICHA ZA MNATO NA VIDEO KWA AJILI YA KAMPUNI YA EACOP LTD NCHINI TANZANIA KUMBUKUMBU NA: 00000437

Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) LTD ("EACOP LTD"), inaalika kampuni zenye uzoefu na weledi wa kutosha kuonesha nia ya kutoa Huduma ya Uchukuaji wa kumbukumbu za Picha za mnato na Video kwa ajili mradi wa EACOP nchini Tanzania.

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba la kusafirisha Mafuta lililofukiwa chini ya ardhi linalokatisha mipaka ya nchi mbili litakalo safirisha mafuta ghaa Kwenda katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka rasi ya Chongoleani karibu na Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 296 zitakuwa nchini Uganda na kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:**
Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) LTD ("EACOP LTD"), inaalika kampuni zenye uzoefu na weledi wa kutosha kuonesha nia ya kutoa Huduma ya Uchukuaji wa kumbukumbu za Picha za mnato na Video kwa ajili mradi wa EACOP nchini Tanzania.

- Kutoa huduma za kitaalamu za upigaji picha za mnato kulingana na mahitaji ya kampuni.
- Kutoa huduma za upigaji picha za video, ikijumuisha utayarishaji wa video na uhariri
- Kujumuisha jumbe na chapa ya kampuni katika maudhui ya video.
- Kushiriki katika uundaji maudhii na ubunifu wa mawazo yanayowiana na chapa ya kampuni.
- Kuandaa vibali muhimu na ruhusa kwa ajili kutayarisha video katika maeneo lengwa
- Kutangaza matukio ya kampuni, makongamano na warsha.
- Kupiga picha za matukio muhimu na kutoa mchanganyiko wa picha halisi katika mionekano mbalimbali ya kuvutia
- Kupiga picha za kitaalamu za sehemu ya uso wa kampuni na wana timu
- Kufanya usanifu baada ya utayarishaji, ikijumuisha urekebishaji wa rangi na uhariri
- Kupanga na kuhifadhi nyaraka za kidijitali kwa usalama kwa ajili ya matumizi ya kampuni.
- Kuwezesha wasomaji wa majukwaa ya mtandaoni kutazama na kupakua mafaili

**VIGEZO MUHIMU:**
Makampuni au taasisi zinzoonesha nia zinaalikwa kutuma maombi na kuambatanisha nyaraka zifuatazo:

- Maelezo ya uzoefu, utalaamu na uwezo wa kutoa huduma katika mawanda yanayohitajika
- Maelezo ya kampuni yanahusu huduma zinazotolewa, uthibitisho wa utendaji kazi, pamoja na barua za uthibitisho kutoka kwa wateja watatu walikwisha fanya kazi na kampuni hiyo.
- Leseni ya Biashara.
- Cheti cha usajili toka BRELA (ambatanisha kivuli cha cheti)
- Uthibitisho wa kusajiliwa na Mamlakaya Mapato Tanzania (TRA) na Cheti cha mlipa kodi cha mwaka wahivi karibuni.
- Waombaji wanasisitizwa sana kuhakikisha kuwa wamesajiliwa kwenye kanzidata ya EWURA (LSSP) ya Watoa Huduma za Ugavi wa Ndani, wakati wa kuwasilisha maombi ya kuonesha nia,
- Kukidhi Kanuni za watoa huduma wa ndani za mwaka 2017 na fasili ya Kampuni ya Ndani.
- Uthibitisha wa wasifu wa wafanyakazi mhimu watakaohusika katika kutoa huduma za mradi ikijumuisha vyeti vyao, kiwango cha elimu, uzoefu na uwezo wa kutoa huduma husika
- Uwezo wa kifedha wa kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kuwasilisha taarifa za fedha ya miaka mitatu iliyopita.
- Ushahidi wa Mifumo ya Usimamizi wa shirika la QHSE, utaratibu na mchakato kwa mujibu wa viwango vinavyotumika vya ndani na Viwanda kwa kazi zinazofanana.
- Uthibitisho wa kupiga vita rushwa, ufisadi, kwa kuzingatia Haki za Binandamu.

Kampuni zenye nia, ambazo zina uwezo na rasilimali za kutosha kutoa huduma zilizotajwa hapo juu zinapaswa kutuma maombi na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe ya **procurement.tz@eacop.com** (ukubwa wa barua pepe usizidi 20Mb) mnamo au kabla ya saa **11:00 jioni** kwa saa za Afrika Mashariki (EAT) mnamo au kabla ya tarehe **23 Disemba 2023**. Kichwa cha Barua pepe kiwe **00000437 -** Utoaji huduma ya Uchukuaji wa kumbukumbu za Picha za mnato na Video. Maombi yote yakuonesha nia yawe kati ya kurasa 10 hadi 20.

Maombi yote lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kingereza.

**Muhimu:** Kampuni ya EACOP LTD itapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia kulingana na tangazo hili la kuonesha nia na kufanya tathmini kwa kuzingatia vigezo vya ndani ili kubaini kampuni ambazo zitakazojumuishwa kwenye orodha ya makampuni ya awali yenye vigezo. Mwaliko wa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa makampuni ya awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji waTaarifa (NDA). Kampuni ya EACOP LTD inaheshimu haki katika kufanya maamuzi ya kuchagua au kukataa kampuni na kuheshimu maamuzi yake pasipo kutoa sababu kwa kampuni husika.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Timu zetu za taifa zianze maandalizi mapema kujiandaa AFCON, WAFCON

**ZIMEBAKI** wiki tatu kabla ya kuuaga mwaka huu wa 2023 na kuukaribisha mwaka mpya wa 2024 ambao utakuwa na matukio makubwa katika sekta ya michezo kwa nchi yetu.

Mwaka ujao (2024) ni mwaka ambao Tanzania itashuhudia timu zake mbili za soka za taifa zikishiriki katika mashindano makubwa Afrika kwa ngazi ya timu za taifa.

Timu yetu ya taifa ya wanaume, Taifa Stars itashiriki kwa mara ya tatu fainali za Afrika (AFCON) za mwaka 2023 ambazo zimesogezwa mbele na kuchezwa mwakani.

Mbali na Taifa Stars, timu yetu ya wanawake 'Twiga Stars' nayo wiki hii imefuzu kucheza fainali za Afrika zitakazofanyika pia mwakani nchini Morocco.

Kufuzu kwa timu hizi na ushiriki mzuri wa klabu zetu kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na kufika hatua ya makundi ni ishara kubwa kuwa kwa sasa soka la Tanzania linazidi kupanda chati, ni jambo la kujivunia.

Hata hivyo ni vizuri kukumbushana katika kila hatua, kwa sasa timu zetu za taifa zinasubiri kushiriki fainali za Afrika kwa wanaume na wanawake baada ya kufuzu.

Kwa wahusika huu ndio wakati wa kuanza kuziandaa timu hizi nje na ndani ya uwanja ili ziende kufanya vizuri kwenye fainali hizo za Afrika mwakani.

Tusitarajie miujiza kutupa matokeo mazuri kama hatutaandaa timu zetu kikamilifu na kuachana na maandalizi ya zima moto yanayofanyika wiki moja au siku chache kabla ya kuanza kwa mashindano.

Maandalizi haya tunayoyazungumzia sio kutoka kwa Shirikisho la soka Tanzania (TFF) peke yake, bali kwa Serikali na wadau wengine wa timu zetu hizi za taifa.

Huu ndio wakati wa kuunganisha nguvu zetu kwa pamoja kuziandaa timu zetu hizi ili angalau katika fainali hizi za mwakani ziweze kufika mbali na kuondoa uteja wa kuishia hatua za awali.

Kila upande ufanye kazi yake ipasavyo, katika maandalizi kuanzia kwa Shirikisho lenyewe, Serikali kupitia Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo na wadau wengine kuziingiza timu zetu hizi mapema kambini kujiandaa.

Tunafahamu inaweza ikawa ngumu kuwapata wachezaji wote kwa wakati mmoja na kuwaweka kambini kutokana na majukumu yao kwenye vilabu wanavyotoka, lakini bado kuna haja ya kuweka mazingira ya timu hizi kuanza maandalizi ya mapema sana.

Watanzania baada ya kiu yao ya muda mrefu ya kuona tunashiriki fainali hizi kwa mara nyingine, sasa wana kiu ya kuona tunafanya vizuri na kuacha kuwasindikiza wenzetu.

Kwa timu za wenzetu mbali na kuwa na wachezaji wenye ubora na viwango vya juu, pia maandalizi yao yamekuwa nguzo imara ya kufanya vizuri.

Fainali za mwaka 2019 ambazo Taifa Stars ilishiriki haikufanya vizuri baada ya kuondolewa hatua ya awali, tunaamini fainali za mwakani hazitakuwa na matokeo kama hayo, tunaamini maandalizi yataanza mapema na tutapata matokeo mazuri.

Lakini kubwa zaidi ni lazima tuzipongeze timu zetu hizi kwa kufuzu kwa pamoja fainali za hizi za Afrika, zipo nchi nyingi si tu za ukanda huu wa Afrika Mashariki bali Afrika kwa ujumma zimeshindwa kufuzu fainali hizi kwa timu zote, za wanawake na hata wanaume, hivyo kwa Tanzania kufanya hivyo tunapaswa kuzipongeza timu zetu hizi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:**
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

### Wasanii hatujasikia wimbo kwa waathirika wa mafuriko

**MPAKA** sasa hakuna msanii, aliyetunga wimbo wowote wa kutoa salamu za pole kwa waathirika wa mafuriko yaliyotokea usiku wa kuamkia Jumapili huko Katesh katika Wilaya ya Hanang mkoani Manyara.

Nilichosikia ni Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), kutoa wito kwa wasanii kuungana kwa ajili ya kuchangia familia zilizoathirika na mafuriko hayo ambayo watanzania wenzetu wamepoteza maisha.

Jumatano iliyopita Katibu Mtendaji wa BASATA, Dk. Kedmon Mapana, alisema wako tayari kuwasindikiza wasanii wanaotaka kutoa mchango wao kwa waathirika.

Hilo ni jambo zuri, na inawezekana kuna baadhi ya wasanii wakaenda kutoa misaada, haizuiwi, msaada anatakiwa kutoa mtu yeyote yule.

Mvua iliyonyesha usiku wa kuamkia jumapili ilisababisha mafuriko ya tope zito kutoka maeneo ya mlimani, lililoshuka chini na kusambaa kwa kasi kubwa kwenye makazi ya watu na kusababisha vifo, kuharibu mali na miundo mbinu.

Serikali imeonekana kuwa bega kwa bega na waathirika katika kipindi chote kigumu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, alikatisha ghafla ziara yake nchini Dubai na kurejea haraka nchini kuungana na wananchi wake katika kipindi hiki kigumu ambapo alielekea eneo la maafa kuwapa pole wafiwa, kuwafariji waathirika na kuwapa moyo kuwa serikali ipo nao bega kwa bega kwa mahitaji yote ya kibinadamu na kijamii hasa kwa kipindi hiki.

Lakini nimeona pia wanasiasa mbalimbali nao wakienda kuwatakia heri na kuwapa pole wafiwa na huu ndiyo utamaduni wa Watanzania enzi na enzi.

Kila kada huwa inatoa mchango kwa namna yake, wapo wananchi watakaojitolea vyakula, damu, nguo na pesa, hata Waandishi wa Habari wanajitolea kwa kuandika na kuzipa kipaumbele habari za huko ili kuwafanya wananchi na wasamaria wema kuzidi kugushwa na kuendelea kutoa misaada.

Bado naona tasnia ya muziki haijafanya ya kazi yake vizuri, nilitegemea mpaka sasa baadhi ya wasanii wangekuwa wameshatoa nyimbo kwa ajili ya kuwapa pole na kuwafariji waathirika.

Hili wala lisingekuwa jambo la ajabu, wanamuziki wa zamani walifanya sana kazi hii, kwani wao chochote kinachotokea ambacho kinalihusu taifa hasa jambo zito kama hili, bendi zingekuwa zimeshaingia studio kutoa nyimbo.

Huu ungekuwa sehemu ya mchango wa wasanii na wanamuziki kwa waathirika wa Katesh.

Hata wakati wa vita ya Nduli Idd Amin mwaka 1978 hadi 1979, wanamuziki hawakupigana vita, lakini nyimbo zao zilikuwa ni silaha tosha kwa adui.

Miaka ya 1970, kulitokea mafuriko makubwa Rufiji mkoani Pwani, wanamuziki waliingia studio na kutoa nyimbo za kuwapa pole wafiwa.

Labda anaweza kutokea mtu akasema enzi zile bendi zilikuwa zikirekodi bure kwenye studio za RTD na sasa kurekodi imekuwa ni gharama, msanii anatakiwa kutoa pesa zake mfukoni, lakini hadi leo hii studio za Redio ya Taifa zipo.

Nadhani sasa BASATA ingeongea na TBC ili wasanii, na wanamuziki wanaotaka kurekodi nyimbo kwa ajili ya majanga au matukio ya kitaifa iwe bure kwa sababu wanafanya hivyo kwa ajili ya taifa.

Kuna dhana inajengwa kuwa wasanii wa sasa si wabunifu, na uwezo wao ni nyimbo za mapenzi tu, lakini nao wanakataa wakidai hawawezi kutoa pesa zao mfukoni, wale wa zamani walikuwa wanarekodi bure.


BASATA ingeweza kukusanya hata wasanii kina Diamond, Ali Kiba, Harmonize, Mbosso na wengine wengi na kutoa nyimbo mbili au tatu zinazohusiana na maafa hayo, wakaingia studio za TBC wakarekodi zikaingia sokoni na pesa ambazo zingepatikana zingepelekwa kwa waathirika.


Wala haitokuwa ajabu, kwani mwaka 1985, wanamuziki mastaa nchini Marekani wakiongozwa na Michael Jackson na Lionel Richie walifyatua singo iitwayo 'We Are the World' iliyouza zaidi ya nakala milioni 20 kwa ajili ya kusaidia watoto masikini wa Afrika.




# MIAKA 62 YA UHURU

## (1961 - 2023)









JUMAMOSI DESEMBA 9, 2023

NIPASHE

# Kutoka Nyerere Ujamaa hadi Kazi Iendelee

**Na Mwandishi Wetu**

KILA zama na kitabu chake. Msemo huo unasadifu na awamu sita za uongozi wa nchi tangu uhuru wa Tanganyika mwaka 1961 hadi sasa serikali ikiwa chini ya awamu ya sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan. Kuanzia awamu ya kwanza, chini ya Rais wa Kwanza, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere hadi sasa, kumekuwa na falsafa tofauti katika kila awamu.

Baada ya kupatikana kwa uhuru kutoka kwa wakoloni wa Kiingereza, nchi ilikuwa katika matatizo makubwa ya kiuchumi huku huduma za kijamii zikiwa duni. Uchumi wa nchi ulikuwa chini ya watu wachache huku wananchi wengi wakiwa hohehahe.

Hapo ndipo baada ya Uhuru, baadaye Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ulioanzisha taifa la Tanzania mwaka 1964, serikali ilichukua uamuzi mgumu wa kutaifisha mali zote zilizokuwa chini ya mabepari na kuwa mikononi mwa serikali. Hapo ndipo Azimio la Arusha lilipoanzishwa mwaka 1967 na kuibuka kwa Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea.

Kupitia Azimio la Arusha, njia kuu za Uchumi zilimilikiwa na wananchi chini ya serikali yao. Taasisi zilizokuwa chini ya watu binafsi ziliwekwa mikononi mwa umma. Mipango ya Maendeleo ya Taifa iliandaliwa pamoja na maazimio mbalimbali yakiwamo Azimio la Iringa la Siasa ni Kilimo lilianzishwa mwaka 1972 na Azimio la Musoma la Elimu kwa Wote mwaka 1974.

Serikali ya awamu ya kwanza, kazi yake kubwa ilikuwa kuweka misingi imara ya Uchumi kwa maendeleo ya taifa ili kuitoa nchi kutoka katika matatizo kama vile ujinga, maradhi na umaskini yaliyoitwa 'maadui watatu wa taifa.'

Serikali pia iliibua kaulimbiu mbalimbali ambazo zilihamasisha jamii kufanya kazi kwa bidii ili kujiletea maendeleo pamoja na sekta mbalimbali. Nyerere alitoa mwelekeo wa maendeleo huku akisisitiza kuwa ili taifa lipige hatua kimaendeleo linahitaji watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora. Aliamini kwamba vitu hivyo ni vya msingi katika kuliletea taifa maendeleo ya kweli.

Mashirika mbalimbali yalianzishwa huku yale yaliyokuwa yametaifishwa yakiimarishwa. Viwanda mbalimbali vikiwamo vya nguo na kuongeza thamani ya mazao vilianzishwa na kutoa ajira kwa Watanzania wengi.

Pamoja na mipango hiyo mizuri, Tanzania ilikumbwa na matatizo ya kiuchumi yaliyotokana na kupanda kwa bei ya mafuta katika soko la dunia pamoja na kuporomoka kwa sarafu ikilinganishwa na dola ya Marekani. Nchi pia iliingia katika vita na Uganda mwaka 1978 ambavyo vilisababisha kuporomoka kwa hali ya uchumi.

**MWINYI NA RUKHSA**

Baada ya Nyerere kung'atuka mwaka 1985, Mzee Ali Hassan Mwinyi alichukua uongozi huku hali ya ucuhumi ikiwa mbaya. Bidhaa zilipatikana kwa shida na hata zilipopatikana zilikuwa kwa njia ya magendo na ulanguzi. Hali hiyo ilianza wakati wa Nyerere hadi kufikia hatua ya kutangaza vita dhidi ya ulanguzi na uhujumu Uchumi iliyoongozwa na Hayati Edward Moringe Sokoine.

Kutokana na kuwapo kwa hali hiyo, serikali ya awamu ya pili chini ya Mzee Mwinyi, ilianzisha mageuzi ya kiuchumi ambayo pamoja na mambo mengine, yalitoa fursa ya upatikanaji wa bidhaa kwa njia za uwazi na kuruhusu maduka ya watu binafsi kuuza bidhaa kwa bei stahiki.

Pamoja na kutoa Rukhsa hiyo, Mwinyi alisisitiza uwajibikaji kwa watu waliopewa dhamana ya kuongoza taasisi na mashirika ya umma. Kwa wale wasiowajibika, waliondolewa kwenye nafasi zao kupitia msemo maarufu wa 'FAGIO LA CHUMA' kwamba ukizembea au usipotimiza wajibu wako utakumbwa na 'Fagio la Chuma.

Katika kipindi hicho pia yalishuhudiwa mageuzi makubwa ya kiuchumi kwa kuruhusu sekta binafsi kushiriki katika kujenga uchumi - kutoka Uchumi hodhi kwenda uchumi wa soko. Mwaka 1992 Azimio la Zanzibar lilitoa mwelekeo mpya kwa kuruhusu pia viongozi wa umma kuwa na hisa katika kampuni au mashirika binafsi tofauti na ilivyokuwa Azimio la Arusha.

Maduka ya kubadilisha fedha za kigeni yalifunguliwa huku baadhi ya taasisi kama vile benki zikiuza hisa, kampuni na mashiriki yasiyotoa faida kufungwa na maelfu ya wafanyakazi kupunguzwa kazi. Lililokuwa Shirika la Utalii Tanzania (TTC) wakati huo ambalo lilikuwa likimiliki hoteli mbalimbali maduka ya bidhaa za kitalii na kitamaduni, kwa mfano lilivunjwa na kuundwa Bodi ya Utalii Tanzania (TTB).

Kampuni mbalimbali kama za Bia (TBL) na Sigara (TTC) zilibinafsishwa kupitia mpango wa kuimarisha uzalishaji kwa kuingia ubia na wawekezaji wapya . Yote hayo yalifanywa kwa maelekezo ya mashirika ya fedha ya kimataifa - Benki ya Dunia (WB) na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) kupitia sera iliyojulikana kama 'Structural Adjustment Program (SAP).

Sera hiyo pamoja na mambo mengine, ilitaka serikali kujiondoa katika uendeshaji wa uchumi badala yake ibaki na jukumu la udhibiti, kutunga sheria, sera na miongozo ambayo itasimamia ushiriki wa sekta binafsi na wadau katika Uchumi. Msisitizo mkubwa ulikuwa kuiwezesha sekta binafsi kuwa mhimili mkuu katika ukuaji wa uchumi.

**UWAZI NA UKWELI**

Awamu ya tatu chini ya Benjamin Mkapa iliingia madarakani mwaka 1995 wakati mageuzi ya kiuchumi yakiendelea. Ubinafishaji wa mashirika na taasisi mbalimbali uliendelea ikiwamo iliyokuwa Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) ambayo ilizaa benki za NBC Limited, National Microfinance Bank (NMB) chini ya serikali kwa asilimia 100 na National Bureau de Change baadaye Twiga Bancorp pia chini ya serikali.

INAENDELEA UK 10




# OSHA yajivunia mafanikio ndani ya miaka mitatu

**Na Mwandishi Wetu**

WAKALA wa Usalama wa Afya Mahali pa Kazi (OSHA) umesema katika kipindi cha miaka mitatu umepata mafanikio ikiwamo kuboresha utendaji wa kazi.

Mkurugenzi Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam katika kikao kazi baina yake na wahariri pamoja na waandishi wa habari.

Kabla ya wakala huo kuanzishwa, usimamizi wa usalama na afya mahali pa kazi ulikuwa ni kitengo chini ya idara ya kazi kilichojulikana kama Kitengo cha Ukaguzi wa Viwanda.

Khadija alisema kutokana na mabadiliko ya kisiasa, teknolojia, masuala ya utandawazi na ukuaji wa uchumi, ilibainika kwamba mabadiliko yaliambatana na vihatarishi vipya katika ulimwengu wa kazi.

Alisema vihatarishi hivyo vilihitaji mbinu mbadala kukabiliana navyo, na hivyo kupelekea uhitaji wa kuhuisha ama kufuta baadhi ya sera za nchi.

Khadija alisema mabadiliko hayo ya sera yalisababisha kufanyike mapitio ya sheria ya ukaguzi wa viwanda na kubaini mapungufu ambayo yalihitaji maboresho.

Aliyataja baadhi ya mapungufu hayo ya sheria yaliyopelekea marejeo hayo kuwa ni pamoja na sheria kujikita kusimamia suala la usalama pekee ambapo suala la athari za kiafya kwa wafanyakazi halikuzingatiwa.

Alisema sheria hujikita kusimamia usalama katika maeneo ya viwanda pekee, badala ya sehemu zote za kazi ambazo nazo pia zina vihatarishi mbalimbali.

Alisema sheria kutozingatia ubora wa huduma inayotolewa, sheria kutozingatia masuala ya mafunzo, uhamasishaji na utunzaji wa takwimu za masuala ya usalama na afya, ndio msingi katika kujenga utamaduni wa kujikinga na magonjwa, ajali na vifo vinavyoweza kutokea mahali pa kazi.

Alisema hivi karibuni mabadiliko yaliyofanyika kwenye miundo ya wizara suala la uwekezaji limepewa kipaumbele na kuhamishiwa katika Ofisi ya Rais.

Alisema OSHA ni taasisi wezeshi, hivyo jukumu lake ni kuhakikisha uwekezaji unakuwa na tija na manufaa kwa wananchi na kulinda nguvu kazi ya taifa ili kuwa na uzalishaji endelevu.

Khadija alisema katika kusimamia hilo, wameweza kufanya maboresho ya kuondoa au kupunguza ada za huduma mbalimbali.

Vilevile, alisema kama taasisi wezeshi, walifanya mapitio ya mlolongo wa shughuli za OSHA na kubaini maeneo yaliyohitaji maboresho katika utoaji wa huduma.

Alisema miongoni mwa maeneo yaliyoonekana kuwa na uhitaji wa maboresho ilikuwa ni kupunguza au kuondoa baadhi ya ada za huduma ambazo zisingeathiri usimamizi na utoaji wa huduma za usalama na afya mahali pa kazi.

"Rais Samia Suluhu Hassan aliridhia ada hizo kufanyiwa marekebisho kwa kufuta na kupunguza ada 13, amependekeza Sh. bilioni 35 zitumike kuimarisha mifumo ya kulinda wafanyakazi ili waweze kuzalisha kwa tija," alisema.

Alisema ada zilizofutwa ama kupunguzwa na OSHA zimeleta unafuu na kuchochea ukuaji wa biashara, uwekezaji nchini na kuongeza ajira kwa Watanzania.

Alizitaja ada walizoondoa kuwa ni usajili wa eneo la kazi iliyokuwa ikitozwa kati ya Sh. 50,000 hadi Sh.milioni 1.8, ada ya fomu ya usajili sehemu za kazi iliyokuwa ikitozwa Sh. 2,000 na kufuta faini za ukosefu wa vifaa vya kuzimia moto ya Sh. 500,000.

Nyingine alizitaja ni ada ya leseni ya ithibati iliyokuwa inatozwa Sh. 200,000 kwa mwaka, ada ya ushauri wa kitaalamu wa usalama na afya ya Sh. 450,000 na ya mafunzo ya elimu kwa umma iliyokuwa inatozwa kiasi cha Sh. 250,000 kwa kila mshiriki.

"Ada ya kipimo cha mzio iliyokuwa ikitozwa Sh. 25,000 kwa mfanyakazi na ada ya kipimo cha kilele cha upumuaji iliyokuwa ikitozwa Sh. 10,000 kwa mfanyakazi.

"Kuondoa ada ya ukaguzi wa usimikaji wa pampu za gesi kwa kila kituo ambayo ilikuwa inatozwa Shilingi 20,000 kwa kila pampu.

Alizitaja ada zilizopunguzwa ni ya uchunguzi wa ajali iliyokuwa ikitozwa Sh.500,000 mpaka Sh. 120,000, ada ya huduma za ukaguzi wa mifumo ya umeme katika vituo vya mafuta vilivyopo vijijini kutoka Sh. 650,000 hadi Sh. 150,000.

Aliyataja mafanikio mengine kuwa ni OSHA kusimika mfumo wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwa ajili ya kutoa huduma, usimamizi wa taarifa za ukaguzi nchini, ajali na mafunzo.

Aliyataja mafanikio mengine kuwa ni OSHA kusimika mfumo wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwa ajili ya kutoa huduma, usimamizi wa taarifa za kaguzi nchini, ajali na mafunzo.

Alisema kupunguza muda wa kupata cheti cha usajili wa sehemu za kazi kutoka siku 14 hadi siku moja kwa kuwa usajili unafanyika kwa njia ya kielektroniki na kutoa leseni ya ithibati ya usalama na afya mahali pa kazi kutoka siku 28 hadi siku saba kwa sasa.

Pia alisema OSHA inashiriki kikamilifu katika miradi ya kimkakati inayotekelezwa na serikali ukiwamo wa Kufua Umeme wa Bwawa la Mwalimu Nyerere, reli ya kisasa ya (SGR), bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima nchini Uganda hadi Tanga na upanuzi wa bandari.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME YA USHINDANI




Maadhimisho ya **MIAKA 62** ya Uhuru wa Tanzania Bara



**Makamishna, Menejement na Wafanyakazi wa FCC, tunaungana na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Watanzania wote katika Maadhimisho ya miaka 62 ya Uhuru wa Tanzania Bara.**

Anuani ya Makao Makuu Dodoma; Mkurugenzi Mkuu, Tume ya Ushindani: Ghorofa ya 6, Jengo la PSSSF, Barabara ya Makole, S. L. P 2351 Dodoma Simu: +255 26 2329087

FCC *Kwa utendaji wa haki katika uchumi wa soko*

info@fcc.go.tz / www.fcc.go.tz

The Fair Competition Commision

fcc_Tanzania

FCC-Fair Competition Commision

@fcc_Tanzania

CALL TOLL FREE NUMBER

0800110094

# Kutoka Nyerere Ujamaa hadi Kazi Iendelee

INATOKA UK 8

Sambamba na kuendelea na mageuzi ya kiuchumi, serikali ilianzisha mpango mahsusi wa kuongeza mapato kupitia kodi ikiwamo kuziba mianya ya ukwepaji kodi na rushwa. Tume ya Kuchunguza Mianya ya Rushwa chini ya Jaji Joseph Warioba, maarufu kama Tume ya Warioba ilianzishwa matokeo ya yote hayo ni baadhi ya vigogo kufikishwa mahakamani.

Katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato, kulikuwa na mafanikio makubwa ambayo yalisaidia ukuaji wa Uchumi na serikali kufanikiwa kulipa madeni ya ndani na nje iliyokuwa inadaiwa. Watu walilalamika ukosefu wa fedha mifukoni, uliopewa jina la UKAPA, lakini Rais Mkapa alisimama imara na kusema anafanya hivyo ili kuimarisha uchumi.

Wakati huo wa uongozi wa awamu ya tatu, kulishuhudiwa ujenzi wa miundombinu ya elimu kupitia Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) na ule wa Elimu ya Sekondari (MMES) ambao kwa kiwango kikubwa ulitekelezwa na serikali ya awamu ya nne chini ya Dk. Jakaya Kikwete.

Pia kasi ya ujenzi wa barabara za lami kuunganisha mikoa yote nchini ilishamiri. Hatua hiyo ilichochea ukuaji wa Uchumi wa maeneo mbalimbali na usafiri na usafirishaji wa bidhaa kutoka mashambani kwenda kwenye masoko.

## ARI MPYA, NGUVU MPYA, KASI MPYA

Mwaka 2005, Tanzania iliingia katika awamu ya nne ya uongozi. Safari hii aliyeshika kijiti cha kuipeleka Tanzania katika hatua nyingine alikuwa Jakaya Kikwete. Wakati akijinadi kutaka kuteuliwa na chama kushika nafasi hiyo, alikuwa na Kaulimbiu ya 'Ari Mpya, Nguvu Mpya, Kasi Mpya, Tanzania Yenye Neema Yawezekana'.

Baada ya kuingia madarakani Desemba, 2005 Kikwete aliahidi kuendeleza mema yaliyofanywa na watangulizi wake katika uchumi, siasa na huduma za kijamii. Ni chini ya uongozi wake ilipotekelezwa MMES kwa kujengwa shule nyingi za sekondari ngazi ya kata zilizotoa fursa kwa watoto wengi kujiunga na elimu ya sekondari.

Kikwete pia aliendeleza ujenzi wa miundombinu ya barabara kwa kiwango cha lami kuunganisha mikoa. Kama ilivyokuwa wakati wa Mkapa na kabla yake, hali ya barabara ilikuwa mbaya na wananchi walipata shida. Kutoka Dar es Salaam kwenda Lindi na Mtwara; Mtwara- Masasi - Songea hadi Mbamba Bay; Tunduma - Sumbawanga hadi Mpanda; Iringa - Dodoma - Manyara hadi Minjingu; Dodoma-Singida hadi Mwanza zilikuwa shida kupitika hasa wakati wa mvua.

Mtu alipoamua kusafiri kikazi au kwa dharura, alikuwa akipata mawazo mazito ni namna gani atapita katika njia hizo na zingine. Kwa sasa hali hiyo ni historia kwani usafiri katika maeneo mengi ni mzuri kutokana na kasi ya ujenzi wa Barabara tangu awamu ya tatu hadi sasa.

Sambamba na elimu, serikali chini ya Rais (mstaafu) Kikwete ilianzisha mageuzi ya sekta ya afya kupitia Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM). Kupitia mpango huo, iliazimiwa kuwa kila Kijiji kiwe na zahanati na kata kuwa na kituo cha afya huku wilaya ikiwa na hospitali na mkoa hospitali ya rufani. Mageuzi hayo katika sekta ya afya yameleta ahueni kubwa kwa wananchi.

Rais Kikwete pia aliingia madarakani wakati hali ya kisiasa ikiwa si nzuri kwa upande wa Zanzibar, aliouita 'Mpasuko wa Kisiasa Zanzibar'. Tatizo hili lilifanyiwa kazi kwa kiasi kikubwa na kuleta maelewano kati ya pande zilizokuwa zikihasimiana kwa maana ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Chama cha wananchi (CUF).

Majadiliano baina ya pande husika yalimaliza kwa kiasi kikubwa tofauti za kisiasa na uhasama miongoni mwa Wazanzibari ambao walikuwa hawashirikiani hata katika masuala ya kijamii. Matokeo ya mchakato huo yaliwezesha kuanzishwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK).

## HAPA KAZI TU

Dk. John Pombe Magufuli aliingia madarakani mwaka 2015 huku akiwa na kaulimbiu ya HAPA KAZI TU - kila mtu lazima afanye kazi kwa bidii ili kujiletea maendeleo. Alisisitiza hata viongozi waliopewa dhamana ya uongozi katika nafasi mbalimbali, wafanye kazi kwa ajili ya kuwahudumia wananchi.

Kupitia kauli yake hiyo pia, alikuwa na kauli ya KUTUMBUA MAJIPU kwa maana ya kuwafukuza kazi viongozi wote katika ngazi mbalimbali ambao watashindwa kutekeleza majukumu yao na kujihusisha na rushwa na ubadhirifu. Alikuwa mkali dhidi ya watu waliojihusisha vitendo vya rushwa, ubadhirifu na ukwepaji kodi.

Enzi za Magufuli pia ilishuhudiwa kasi ya ukusanyaji mapato ikiongezeka kwa kuwataka wafanyabiashara wote kulipa kodi stahiki. Pia alianzisha mfumo wa ulipaji kodi kielektroniki huku akiwasisitiza wafanyabiashara kutoa risiti za mauzo ya bidhaa husika na wananchi kudai risiti pindi wanaponunua bidhaa.

Ujenzi wa miundombinu ya barabara kama ilivyokuwa chini yake akiwa Waziri wa Ujenzi awamu ya tatu na ya nne, pamoja na reli ya kisasa (SGR) vilipamba moto wakati wa uongozi wake.

Pamoja na kufanya mambo yote hayo, serikali yake ililalamikiwa kwa kuminywa kwa dekomrasia, haki za binadamu na uhuru wa kujieleza baada ya kutunga sheria zilizoonekana kandamizi.

Mikutano ya kisiasa kwa vyama vya upinzani ilipigwa marufuku na

INAENDELEA UK 15




# Sekta ya elimu ilivyong'ara miaka 62 ya Uhuru Tanzania

**Na Mwandishi Wetu**

TANZANIA leo inaadhimisha miaka 62 ya Uhuru wa iliyokuwa Tanganyika (sasa Tanzania Bara) huku ikivijivunia maendeleo ya sekta ya elimu katika muda wote huo. Maendeleo hayo yanabainishwa na ongezeko la shule za msingi hadi sekondari kwa maana ya kidato cha kwanza hadi cha sita, vyuo vya ufundi, vyuo vya kati na vyuo vikuu.

Maendeleo hayo yanaakisi na dhana halisi ya kwamba taifa lolote lisilo na rasilimali watu wenye elimu na ujuzi wa kutosha ni sawa na taifa mfu. Rasilimali ni kichocheo kikubwa katika taifa lolote ili kufikia malengo halisi ya maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Kutokana na dhana hiyo, ndiyo maana Mwalimu Julius Nyerere katika Kitabu cha Nyerere Kuhusu Elimu alisema: "Elimu tunayoitoa, kwanza ni lazima ikomboe Mtanzania kifikra kisha kutawala na kuyatumia mazingira; na kuisaidia jamii inayomzunguka."

Maana halisi ya Nyerere kuhusu elimu, kwa mujibu wa kauli hiyo, ni kumpa mwanadamu uwezo wa kujikomboa - kujitambua kifikra na kuyatumia vyema mazingira yanayomzunguka kwa maana ya fursa kwa maendeleo yake na ya jamii yake. Kubwa zaidi, kusaidia jamii kujikomboa dhidi ya maadui umaskini, ujinga na maradhi kwa kutoa mchango wake wa kitaaluma, mawazo na hali na mali.

Hali hiyo ni tofauti na wakati wa ukoloni. Elimu wakati wa ukoloni ilikuwa lengo la kuwafundisha watu kutumikia utawala wao badala ya kujenga uwezo wa kujitegemea. Elimu ilikuwa inatolewa kwa watu wachache watoto wa machifu na wale waliokuwa wakiishi mijini. Kwa mantiki hiyo watu wengi walikosa fursa, hivyo kukabiliwa na umaskini mkubwa.

Baada ya kupata uhuru, serikali iliweka msisitizo mkubwa katika kuboresha na kusambaza elimu kwa wananchi wake. Mfumo wa elimu uliboreshwa na kuwa huru na wa kutegemea mahitaji ya taifa, hivyo ikapitishwa sera ya kutoa elimu bure na msingi, na kuongeza fursa za elimu kwa wote.

Shule za msingi zilijengwa zaidi miaka ya 1970 ili kuwezesha watoto wengi zaidi wa kizalendo kupata elimu ya msingi. Hapo ndipo falsafa ya Elimu ya Kujitegemea iliyokuwa sehemu ya Azimio la Arusha ilianzishwa kwa lengo kwamba licha ya elimu ya darasani pia mwanafunzi apate maarifa za kufanya kazi za mikono. Katika shule nyingi za vijijini, kupitia Elimu ya Kujitegemea, wanafunzi pia walishiriki kazi za mikono kupitia miradi ya shule kama kilimo na mifugo.

Aidha, mwaka 1974 lilianzishwa Azimio la Musoma kuhusu Elimu kwa Wote kwamba kila mtoto aliyefikisha angalau miaka saba ajiunge na elimu ya msingi. Hatua hiyo pia iliwezesha watoto wengi kujiunga na shule za msingi na miaka michache baadaye, kukawapo ongezeko la wahitimu wa elimu ya msingi tofauti na ilivyokuwa awali.

Pamoja na jitihada hizo za serikali kutoa elimu ya msingi kwa Watoto wengi, changamoto kubwa ilikuwa nafasi finyu za kujiunga na elimu ya sekondari. Sababu kubwa ni kwamba shule za sekondari zilikuwa chache, hivyo kushindwa kutosheleza mahitaji ya vijana wengi kupata fursa hiyo.

Katika mkoa wa Iringa, mathalan, shule zilizokuwapo wakati huo ni Malangali, Njombe, Tosamaganga, Ifunda, Lugalo zilizokuwa zikipokea wanafunzi wa kiume na Iringa Wasichana kwa ajili ya wanafunzi wa kike pekee. Wengine waliokuwa wakipata fursa hiyo, walikuwa wakijiunga na shule za Iyunga, Rungwe na Loleza (Mbeya), Songea Wavulana na Wasichana na Tunduru (Ruvuma), Msalato, Mpwapwa, Bihawana na Mazengo (Dodoma), Mzumbe, Kilakala na Ifakara (Morogoro).

Kadhalika, nafasi za kujiunga na kidato cha tano zilikuwa finyu kwa kuwa shule zilizokuwapo wakati huo zilikuwa chache. Pia waliofaulu kidato cha sita, hawakuchaguliwa wote kujiunga na elimu ya juu kutokana na ukweli kwamba vyuo vilivyokuwapo vilikuwa vichache.

**MAGEUZI MAKUBWA**

Kutokana na changaoto hizo, serikali katika awamu ya uongozi chini ya Rais Benjamin Mkapa (marehemu), ilianzisha Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) ambao lengo mahususi lilikuwa kuongeza udahili wa watoto wenye umri wa kuanza elimu ya msingi baada ya kubainika kwamba wengi walikosa nafasi hiyo kwa sababu ya uhaba wa shule.

Serikali, kupitia mpango huo, ilijenga shule nyingi mpya na kupanua zilizokuwapo kupitia fedha za msamaha wa nchi maskini zilizolemewa na madeni (HIPC). Ndani ya muda mfupi baada ya kuanza kwa mpango huo, kulikuwa na ongezeko la wanafunzi waliodahiliwa kwa zaidi ya asilimia 100.


Mpango huo pia ulikwenda sambamba na ujenzi wa matundu ya vyoo, nyumba za walimu, majengo ya utawala, ununuzi wa vitabu vya kiada na ziada, na ajira kwa walimu ili kukidhi mahitaji halisi.


Ongezeko hilo lilisababisha wanafunzi wengi waliomaliza elimu ya msingi kukosa nafasi za kujiunga na elimu ya sekondari sababu kubwa ikiwa ni uhaba wa shule za kudahili wanafunzi wote wenye sifa za kujiunga na ngazi hiyo ya elimu.

Serikali ya awamu ya tatu ikiwa uongozi kumaliza muda wake, na kupitia Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2005-2010, ilianzisha Mpango wa Maendeleo ya Sekondari (MMES).

Mpango huo uliazimia kwamba kwa kuanza, kila kata kuwa na shule ya

Inaendelea uk. 13



# Sekta ya afya imeupiga mwingi

**Na Mwandishi Wetu**




AFYA ni msingi mkuu wa ustawi wa jamii yoyote kiuchumi, kisiasa na kijamii. Ili taifa lolote lipige hatua za maendeleo, linapaswa kuwa na jamii iliyo na afya bora.

Kama watu katika jamii husika wana afya mgogoro, ni dhahiri kwamba maendeleo hayawezi kupatikana. Kwa maneno mengine, hakuna tija katika kilimo, viwanda na biashara kama hakuna afya bora. Hata familia haiwezi kuzalisha au kutekeleza majukumu kwa ufanisi ikiwa mmoja wao ni mgonjwa.

Kwa kutambua hilo, serikali imekuwa kila mwaka ikiwekeza kiasi kikubwa cha fedha katika sekta ya afya ili kuhakikisha sekta zingine za kiuchumi na kijamii zinapiga hatua kimaendeleo.

Ikiwa leo Tanzania inaadhimisha miaka 62 tangu kupatikana kwa iliyokuwa Tanganyika, kumekuwa na maendeleo makubwa katika sekta ya afya, hayo yote ni katika kuonyesha kwamba afya ni jambo la kipaumbele kwa kila eneo la uzalishaji na utoaji huduma.

Tangu awamu ya kwanza ya uongozi wa nchi chini ya Mwalimu Julius Nyerere hadi sasa chini ya Rais Samia Suluhu Hassan, sekta ya afya imepiga hatua kubwa kuanzia miundombinu ya utoaji wa huduma hadi huduma zenyewe bila kusahau ongezeko la watumishi wakiwamo madaktari, madaktari bingwa, wauguzi na wataalamu wa dawa na maabara.

Mara tu baada ya kupata Uhuru, aliyekuwa Rais wa kwanza, Mwalimu Nyerere, alitamka bayana kwamba maradhi ni miongoni mwa maadui wa maendeleo, hivyo kila Mtanzania alipaswa kusimama imara katika kukabiliana na adui huyo.

Katika kukabiliana na adui huyo, tangu uhuru, kumekuwa na mikakati mbalimbali ya kuboresha huduma za afya zikiwamo utoaji huduma za chanjo kwa watoto chini ya umri wa miaka mitano; kusimamia viwango vya ubora wa huduma za kinga na tiba katika ngazi zote za utoaji huduma za afya; na kuimarisha huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto ili kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi, vifo vya watoto wachanga pamoja na mimba za utotoni.

Mikakati mingine ni kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika ngazi zote za utoaji wa huduma za afya; kuimarisha huduma za lishe hususani kwa watoto wa umri wa chini ya miaka mitano, vijana balehe na wanawake wa umri wa kuzaa; na kuimarisha huduma za afya na usafi wa mazingira ili kudhibiti magonjwa ya kuambukiza, hivyo kupunguza idadi ya wagonjwa katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini.

Serikali pia imeweka mikakati ya kuimarisha miundombinu ya kutolea huduma za afya katika hospitali za rufani za mikoa na kanda, maalum na taifa pamoja na huduma za matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi; na kudhibiti magonjwa ya mlipuko, magonjwa ya kuambukiza na magonjwa yasiyo ya kuambukiza.



**MAGEUZI MAKUBWA**

Katika miaka 62 ya Uhuru, kumekuwa na mageuzi makubwa katika sekta ya afya na ushahidi wa kutosha unaonekana wazi katika jambo hilo. Miaka ya 1960 baada ya uhuru na miaka ya 1970 hadi 1980, kulikuwa na matatizo makubwa katika sekta ya afya hasa upatikanaji wa vituo vya kutolea huduma za afya.

Halikuwa jambo la ajabu kukuta mgonjwa amebebwa kwenye machela akipelekwa zaidi ya kilomita 20 au 30 kwenye kituo cha huduma za afya. Jambo hilo liliendelea kupungua kidogo kidogo na sasa katika baadhi ya maeneo limeanza kuwa historia.

Aidha, watu wengi, wakiwamo wajawazito, walikuwa wakifia njiani kutokana na kukosekana kwa vituo hivyo. Wajawazito walilazimika kutembea umbali mrefu kutafuta huduma za afya na wengine kuamua kujifungulia nyumbani hali iliyosababisha madhara kwa wengi, ikiwamo vifo vya wajawazito na watoto wachanga.

Ukosefu wa dawa pia lilikuwa tatizo sugu mijini na vijijini. Hata katika maeneo ambayo vituo vya kutolea huduma za afya vilikuwapo, mgonjwa alikuwa akiandikiwa dawa na kutakiwa kwenda kununua kwenye maduka ya watu binafsi au yale yanayomilikiwa na watumishi

Inaendelea uk. 14

ZRA
ZANZIBAR REVENUE AUTHORITY

MAMLAKA YA MAPATO ZANZIBAR (ZRA)

MAADHIMISHO YA MIAKA 62 YA UHURU

IKIWA NI KATIKA KUADHIMISHA MIAKA 62 YA UHURU WA TANGANYIKA, UONGOZI PAMOJA NA WAFANYAKAZI WOTE WA MAMLAKA YA MAPATO ZANZIBAR (ZRA), WANAUNGANA NA WANANCHI WOTE WA ZANZIBAR NA WATANZANIA KWA UJUMLA KUMPONGEZA MHE. RAIS WETU, **DK SAMIA SULUHU HASSAN** PAMOJA NA KUMUOMBEA KHERI NA FANAKA KATIKA KUIONGOZA TANZANIA NA KUILETEA MAENDELEO.

ILI KUFIKIA MAENDELEO HAYO, ZRA INAENDELEA KUWASISITIZA WAFANYABIASHARA KUENDELEA KUTUMIA MFUMO WA KUTOLEA RISITI ZA KIELEKTRONIKI (VFMS) PAMOJA NA KUTOA RISITI WANAPOFANYA MAUZO YA BIDHAA AU HUDUMA PAMOJA NA KUDAI RISITI ZA KIELEKTRONIKI KWA WANUNUZI.

AIDHA, ZRA INAKIRI KUONGEZEKA KWA UWAJIBIKAJI WA HIYARI KWA WAFANYABIASHARA KATIKA MASWALA YA KODI. HEKO KWA VIONGOZI WOTE WA SERIKALI KWA UHAMASISHAJI MKUBWA UNAOENDELEA KUFANYIKA NA MIONGOZO WANAYOITOA AMBAYO INARAHISISHA UKUSANYAJI WA MAPATO NCHINI.

KIPEKEE KABISA, ZRA INAMSHUKURU KWA DHATI RAIS WETU MPENDWA DKT. SAMIA SULUHU HASSAN KUWA MUHAMASISHAJI NAMBARI MOJA WA ULIPAJIKODI WA HIARI AMBAO UMEONGEZA CHACHU KATIKA UWAJIBIKAJI ULIOPELEKEA KUONGEZEKA KWA MAKUSANYO YA KODI.

ZRA INAENDELEA KUIMARISHA MIFUMO YA UKUSANYAJI WA KODI PAMOJA NA KUIMARISHA HUDUMA ZA OFISI ZA MIKOA PAMOJA NA KUCHUKUA HATUA STAHIKI KWA WAFANYA BIASHARA WANAOKWEPA KULIPA KODI NA WATUMISHI WASIOKUWA NA UADILIFU.



"TULIPE KODI KWA MAENDELEO YA ZANZIBAR"

Zanzibar Revenue Authority (ZRA),
P. O, BOX 2072, Mazizini- Zanzibar, Tel: 255-24-2230639/2233041,
Fax: 255-24-2233904, Email: zrb@zanrevenue.org

ZRA Pemba Office
S.L.P 163, Pemba, Zanzibar.
Tel: +255 24 2452553, Fax: +255 24 2452945



# Sekta ya elimu ilivyong'ara miaka 62 ya Uhuru

Inatoka uk. 13

sekondari na kwamba angalau asilimia 50 ya wanafunzi wanaomaliza darasa la saba wajiunge na kidato cha kwanza. Pia iliazimiwa kuwa angalau asilimia 50 ya vijana wanaofaulu kidato cha nne, wajiunge na kidato cha tano na cha sita.

Msisitizo mwingine kupitia MMES, ulikuwa kuongeza ujenzi wa vyumba vya madarasa kwa ajili ya wanafunzi wa kidato cha tano na cha sita, kuajiri walimu wenye shahada, ujenzi wa nyumba za walimu, majengo ya utawala na mabweni.

Hatua hiyo ilishuhudiwa na mafuriko ya wanafunzi katika shule mbalimbali ambao walipata elimu ya sekondari, hivyo kupanua wigo wa maarifa. Watoto wengi wa wananchi wa kipato cha chini walipata fursa tofauti na ilivyokuwa mwanzo.

**ELIMU YA JUU**

Baada ya kupata Uhuru, kilianzishwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambacho kilikuwa sehemu ya Chuo Kikuu cha Afrika Mashariki kabla ya kuwa chuo kikuu rasmi mwanzoni mwa miaka ya 1970. Baadaye kilianzishwa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) mkoani Morogoro ambacho pia awali kilikuwa Kitivo cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

Hatua hiyo ilisababisha wahitimu wachache wa kidato cha sita na wale wenye sifa zinazolingana (equivalent qualifications) kama diploma nao walifanya mitihani ya majaribio kujiunga na chuo kikuu kupata elimu hiyo. Kwa mantiki hiyo, wahitimu wenye shahada walikuwa wachache kutokana na kuwapo kwa vyuo vikuu vichache.

Hata hivyo, kuwapo kwa vyuo vya kati vilivyokuwa vikitoa stashahada ya juu kama Taasisi ya Maendeleo ya Uongozi (IDM) Mzumbe, Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM), Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) na Chuo cha Uhasibu (DSA) pamoja na vyuo vya ufundi vya Dar es Salaam, Arusha na Mbeya vilivyotoa ngazi ya vyeti na diploma, vilisaidia kupatikana kwa wasomi waliochangia maendeleo katika taasisi mbalimbali za umma na binafsi.

Katikati ya miaka ya 1990, mageuzi makubwa yalifanyika kwa kuanzishwa kwa vyuo vikuu vya umma na binafsi ambavyo kwa kiasi kikubwa vilichangia kupatikana kwa kwa wahitimu wenye shahada ya kwanza hadi ya uzamivu. Chuo Kikuu cha Mzumbe kilianzishwa kutoka iliyokuwa IDM na baadaye kuanzishwa kwa vyuo vikuu vishiriki vya elimu vya Mkwawa (MUCE) mkoani Iringa na Dar es Salaam (DUCE) chini ya UDSM.

Aidha kilichokuwa Chuo Kikuu Kishiriki cha Sayansi za Afya Muhimbili (MUCHS) na Chuo Kikuu Kishiriki cha Ardhi (UCLAS) vilivyokuwa chini ya UDSM vilipandishwa hadhi na kuwa vyuo vikuu kamili. Pia Chuo cha Ushirika Moshi ambacho baadaye kilibadilishwa na kuwa Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Stadi za Biashara (MUCOBS) chini ya SUA kilipandishwa na kuwa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MUCOBS).

Mageuzi hayo ya elimu ya juu yaliendelea katika serikali ya awamu ya nne kwa kuanzishwa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) ambacho kina uwezo wa kuchukua wanafunzi 40,000 kwa ujumla.

Mbali na vyuo vikuu hivyo, vyuo vya kati kama IFM, CBE, DSA na Uhasibu Arusha, Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini (IRDP) Dodoma ambavyo vilikuwa vikitoa elimu ngazi ya cheti hadi stashahada za juu na za uzamili, sasa zinatoa shahada za kwanza na za uzamili. Vyuo vya Ufundi vya Arudha, Dar es Salaam (sasa Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam- DIT) na Mbeya (sasa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya - MUST) navyo vinatoa elimu katika ngazi za shahada.

Vyuo hivyo pia vimeanzisha kampasi katika mikoa mbalimbali ambazo kwa kiasi kikubwa zimechangia kuongezeka kwa idadi ya watumishi wa ngazi ya shahada na kuendelea, hivyo kuifanya Tanzania kuwa na rasilimali watu ya kutosha.

**SEKTA BINAFSI**

Katika maendeleo ya sekta ya elimu, sekta binafsi haijaachwa nyuma kwa kuwa na shule kuanzia ngazi ya awali, msingi na sekondari pamoja na ufundi na vyuo vikuu. Mchango wake katika elimu umekuwa wa kupigiwa mfano. Watu, kampuni binafsi na mashirika ya dini yamechangia kwa kiasi kikubwa katika maendeleo ya sekta hiyo.

Ngazi ya elimu ya juu kwa mfano, mashirika ya dini kwa maana ya makanisa, yameanzisha vyuo vikuu katika maeneo mbalimbali ya nchi, hivyo kuchangia ongezeko la udahili wa wanafunzi wa ngazi ya shahada na kuzalisha pia wahitimu wa shahada za umahiri na za uzamivu (PhD).

Kanisa Katoliki kwa mfano linamiliki Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino (SAUT) chenye kampasi kuu Mwanza pamoja na vyuo vikuu vishiriki vya Mbeya, Askofu Mkuu Mihayo (Tabora), Stella Maris (Mtwara), Jordan (Morogoro) na Marian (Bagamoyo) na Mwenge (Kilimanjaro) na Kituo cha Dar es Salaam.

Sambamba na SAUT, kanisa hilo pia linamiliki vyuo vikuu vya Ruaha (RUCU) mkoani Iringa, Afya na Sayansi Bugando (CUHAS- Bugando) na Chuo Kikuu cha Mtakatifu Joseph (SJUIT).

Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) nalo lina vyuo vikuu vya Tumaini Makumira chenye kampasi kuu Usa River, Arusha na vyuo vikuu vishiriki vya Stephano Moshi na KCMC (Kilimanjaro) na Dar es Salaam (TUDARCo). Pia kina Chuo Kikuu cha Iringa (UoI) ma Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Sebastian Kolowa (SEKOMU) Lushoto mkoani Tanga.

Makanisa mengine yanye vyuo vikuu ni Moravian (Kumbukumbu ya Teofilo Kisanji- Mbeya), Anglikana (Mtakatifu Yohana - Dodoma), Waadventisti Wasabato (Chuo Kikuu cha Arusha) na Baptist (Mount Meru- Arusha).

Kwa ujumla, sekta ya elimu imepiga maendeleo makubwa katika miaka 62 ya Uhuru na taifa linajivunia kuwa na wataalamu wa kutosha katika nyanja mbalimbali kwa maendeleo ya nchi kiuchumi na kijamii.



## MIAKA 62 YA UHURU



MRI Mashine

# Sekta ya afya imeupiga mwingi

Inatoka ukurasa 12

wa afya wenyewe.

Kutokana na sekta hiyo kukumbwa na changamoto hizo, mwaka 2007 serikali ilianzisha Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM). Chini ya mpango huo, iliazimiwa kwamba kila kijiji kiwe na zahanati na kituo cha afya katika kila kata na kwamba kijiji ambacho ndipo makao makuu ya kata hakina haja ya kujenga zahanati bali kituo hicho kitakuwa rufani ya ngazi ya zahanati.

Mpango huo pia ulibainisha kwamba katika ngazi ya wilaya kuwe na hospitali ya wilaya na mkoa kuwe na hospitali ya rufani ya mkoa. Pia kuwe na hospitali ya rufani ya kanda katika maeneo mbalimbali na hospitali ya taifa ambayo ni juu ya rufani baada ya zile za kanda.

Mpango huo umefanikiwa kwa kiasi kikubwa kwa kuwa zahanati nyingi zimejengwa katika maeneo mbalimbali vijijini na vituo vya afya kama ilivyokusudiwa. Mpango huo ni endelevu kama inavyoshuhudiwa vituo vya afya vikiendelea kujengwa huku serikali ikitoa mabilioni ya shilingi kutimiza azma hiyo huku wananchi nao wakichangia nguvu zao.

Hatua hiyo imesaidia kupungua kwa vifo vya watoto chini ya umri wa miaka mitano na wajawazito. Kwa mujibu wa takwimu za utafiti wa afya kijiografia (TDHS) mwaka 2022, vifo vya watoto umri chini ya mwaka mmoja vimepungua kwa asilimia 23 kutoka vifo 43 kwa vizazi hai 1,000 vya mwaka 2016 hadi vifo 33 kwa vizazi hai 1,000 mwaka 2022.

Aidha, vifo vya watoto umri chini ya miaka mitano vimepungua kwa asilimia 36 kutoka vifo 67 kwa vizazi hai 1,000 mwaka 2016 hadi kufikia vifo 43 kwa vizazi hai 1,000 katika kipindi hicho.

Wakati leo ni miaka 62 ya Uhuru, kumekuwa na mafanikio makubwa kutokana na ongezeko la vituo vya kutolea huduma za afya ngazi zote kufikia zaidi ya 10,000 ikilinganishwa na 1,343 mwaka 1960. Kati ya vituo hivyo, serikali inamiliki takriban asilimia 70, mashirika ya dini asilimia tisa na iliyobaki ni ya vituo binafsi.

Aidha, mtandao wa vituo vya huduma za afya umepanuka na kusogea karibu zaidi na wananchi zahanati zikikadiriwa kuwa 7,500, vituo vya afya 926; na hospitali za wilaya na halmashauri zaidi ya 180, hospitali zingine 151. Hospitali za rufani za mikoa 28, ngazi ya kanda sita, hospitali za ubingwa maalumu ni tano na hospitali ya taifa ni moja ambayo ni Muhimbili.

Sambamba na ongezeko hilo la vituo vya kutolea huduma za afya, huduma za matibabu zikiwamo za kibingwa zimeimarishwa zikiwamo za vipimo maalum hadi ngazi ya mikoa ambavyo awali vilikuwa vikipatikana katika hospitali za kanda na zile za mashirika ya dini au binafsi kama Aga Khan na Hindu Mandal.

Kukosekana kwa vipimo hivyo, mgonjwa alikuwa lazima achukuliwe sampuli na kupelekwa huko, hivyo kusubiri wiki moja hadi mbili ili virejeshwe. Hali hiyo ilikuwa inasababisha mgonjwa kuendelea kuzidiwa au kupoteza maisha.

Mafanikio mengine yaliyopatikana katika miaka 62 ni ongezeko la idadi ya watumishi katika sekta ya afya. Hali hiyo imesababisha sasa vituo vya afya kufanya hadi huduma za upasuaji mkubwa ambao awali ulikuwa haufanyiki.

Kwa mujibu wa taarifa za Wizara ya Afya, mwaka 2021 wakati nchi inaadhimisha miaka 61 ya Uhuru, wataalamu wa kada mbalimbali za msingi kwenye afya waliosajiliwa waliongezeka hadi takribani 71,365 wakijumuishwa madaktari bingwa, wa kawaida, wauguzi, wataalamu wa maabara, mionzi, wafamasia na mionzi.

Kabla ya uhuru, wataalamu wa kada hizo kwa ujumla wao walikuwa 435. Hali hiyo inaonyesha nchi imepiga hatua kwa kiasi kikubwa na huenda idadi hiyo ikawa imeongezeka ndani ya miaka miwili iliyopita.

**ONGEZEKO LA VYUO**

Katika kuhakikisha wataalamu mbalimbali wa afya wanaongezeka, wakiwamo madaktari bingwa, serikali imepanua wigo wa mafunzo kwa kuanzisha vyuo vya kati vinavyotoa mafunzo katika fani za utabibu, madaktari wasaidizi, uuguzi, maabara na teknolojia ya mionzi.

Pia imepanua udahili wa wanafunzi katika fani za udaktari, uuguzi na famasia katika vyuo vikuu vya serikali, binafsi na nje ya nchi. Miongoni mwa vyuo hivyo ni Muhimbili, KCMC na Bugando.

Pamoja na kuwapo mafanikio hayo, bado kuna changamoto katika baadhi ya maeneo yakiwamo magonjwa ya mlipuko ambayo yamekuwa yakiikumba jamii mara kwa mara na magonjwa yasiyo ya kuambukiza kama vile kansa, shinikizo la damu na kisukari.

Magonjwa hayo yanapaswa kutiliwa uzito wa kipekee kama ambavyo serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi imekuwa ikifanya kampeni za mara kwa mara katika kuyadhibiti kutokana na kugharimu maisha ya watu wengi kwa sasa.



# Kutoka Nyerere Ujamaa hadi Kazi Iendelee

INATOKA UK 10

vyombo vya habari vilizuiwa kuandika maovu yaliyofanywa ndani ya serikali yake.

Hata hivyo, Magufuli alimaliza kipindi cha kwanza cha miaka mitano ya uongozi wake na mwaka mmoja wa ngwe ya pili na kufariki dunia Machi 17, 2021 na nafasi yake kuchukuliwa na Samia Suluhu Hassan, ambaye alikuwa makamu wake.

**SAMIA NA 4R**

Rais Samia baada ya kuingia madarakani, alitoa ahadi nyingi zikiwamo kuleta uhuru wa kujieleza pamoja na kuunda kikosi kazi ambacho kilifanya utafiti na kuibuka na mapendekezo mbalimbali juu ya kuirejesha Tanzania katika mstari wake. Kama ilivyokuwa kwa watangulizi wake, alikuja na msemo wa KAZI IENDELEE.

Pamoja na hayo, Rais alkuja na falsafa ya 4R yaani Reconciliation (maridhiano), Resilience (kuvumiliana), Reforms (mabadiliko) na Rebuilding (ujenzi wa Tanzania mpya) ambazo ni muhimu katika kutatua changamoto zinazoikabili Tanzania kijamii, kiuchumi na kisiasa.

Katika kipindi cha takriban miaka mitatu ya uongozi wake, Rais Samia ameonyesha nia ya dhati katika kuhakikisha nchi inarejea katika misingi ya umoja, amani na mshikamano.

Imeshuhudiwa serikali chini yake ikikutana na viongozi wa vyama vya siasa na kujadiliana masuala mbalimbali huku mikutano ya kisiasa nayo ikirejea tofauti na miaka kadhaa iliyopita. Vyombo vya Habari pia vimepewa uhuru wa kufanya kazi pasipo kuvunja sheria.

Jambo kubwa na la kupigiwa mfano ni hivi karibuni serikali ilipowasilisha muswada wa sheria ya masuala ya siasa inayolenga kufanya mabadiliko katika uchaguzi, vyama vya siasa na kuwapo kwa tume huru ya uchaguzi.


MAADHIMISHO YA MIAKA 62 YA UHURU

zenufa
Dawa Bora...Fahari Ya Watanzania



Rais Wa Jamhuri Ya Muungano Wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan

Bodi ya Wakurugenzi, Mkurugenzi Mkuu, Menejimenti pamoja na Wafanyakazi wa **ZENUFA**, tunaungana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Dkt. Samia Suluhu Hassan** pamoja na watanzania wote katika kuadhimisha miaka 62 ya Uhuru wa Tanganyika

***Dawa Bora Fahari ya Watanzania***

**KAZI IENDELEE**

P.O. Box: 3730, 131/132, Kipawa Industrial Area, Julius Nyerere Road Dar Es Salaam, Tanzania.
Simu: +255 717 305 960

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA

# Mashairi ya Shaaban Robert, Snow-White yalivyotumika kutunga nyimbo za dansi

**Na Adam Fungamwango**

TUMEZISIKIA nyimbo nyingi za zamani, ambazo tunzi zake zilikuwa na maneno murua, mashairi, fasihi na misemo mbalimbali. Pamoja na kwamba wanamuziki wa zamani walikuwa 'vichwa', yaani walikuwa na akili nyingi katika kutafuta maneno ya kupeleka kwenye hadhara, lakini pia wanaonekana walikuwa wanachota maneno kutoka kwenye vitabu vya waandishi mashuhuri wakati huo kama kina Shaaban Robert, Akilimali Snow-White na wengineo.

Zamani watu wengi walikuwa na tabia ya kusoma vitabu mbalimbali vya riwaya na vya mashairi kama ya kina Mathias Mnyampala, Sheikh Amri Abeid Kaluta na wengine kama hao niliowataja juu.

Hata wanamuziki, pamoja na kutunga nyimbo zao, walionekana kuchota baadhi ya maneno kutoka kwenye vitabu vya waandishi hao wa riwaya na mashairi.

Kwa utafiti wangu mdogo tu, nimegundua baadhi ya nyimbo ambazo maneno au vipande vya mashairi vimechotwa kutoka kwenye vitabu mbalimbali vya malenga hao.

Wimbo wa Orchestra Safari Sound ya mtindo wa Dukuduku waliimba wimbo mmoja uitwao 'Gaba'.

Moja kati ya mashairi ya wimbo huo yanasema. "Nimechoshwa eee, nimechoshwa na vituko vyako, afadhali eee, tuachane kwa usalama, ni bora nibaki masikini huru kuliko kuwa tajiri mtumwa papa, sijazeeka bado ningali kijana, nitaolewa, kama ulivyoniona wewe..."



Mwandishi wa vitabu na mshairi, Shaaban Robert, aliyezaliwa 1909 na kufariki 1962. Vitabu vyake mbali na kutumika kwenye vyuo mbalimbali nchini, lakini baadhi ya maneno ya kwenye vitabu vyake na mashairi yametumika pia na wanamuziki mbalimbali nchini kutungia nyumbo zao.

Vipande vya maneno vya wimbo vimetolewa kwenye shairi la Akilimali, kwenye kitabu chake cha Diwani ya Akilimali. Shairi linaitwa 'Enenda Mwana Kunenda', nalo linasema hivi.

"Nimechoshwa na vituko, daima vina nikifu, moyo sinapumziko, bali mwingi usumbufu, Enenda ondoka zako, moyoni unanikifu, enenda mwana kunenda, wendako nisalimie."

Kwenye shairi hilo hilo la 'Enenda Mwana Kunenda', DDC Mlimani Park Orchestra nao walikwenda kuchota kipande cha shairi hilo, na kuliweka kwenye wimbo wa 'Mtu chake Apendacho'.

"Kama mapenzi yaua, kheri potelea mbali, na kama ni kuugua, nitapona siku mbili, enenda nitapumua na kubwa sumbuko hili." Hilo ni shairi.

Sikinde wakachukua kipande kisemacho "Kama mapenzi yaua, kufa sioni muhali. Visa vituko madharau dada na mengi, bila idadi nimevumilia, leo nimefika kikomo naufunga mdomo wangu. Usiponipenda wewe wenzio wanitafuta."

Twende kwenye kitabu kingine cha huyo huyo Akilimali Snow-White, kiitwacho Diwani ya Akilimali kuna shairi lingine liitwalo 'Dunia Rangi Rangile'.

Kuna kipande kimoja cha shairi kimeandikwa hivi. "Dunia kwa mwanaume, yataka kujichumia, kila pembe na ujitume, nawe kujisaidia, siyo ungoje wachume, ukalie kutumia."

Kwa wale mashabiki wa muziki, wanaweza kujua kabisa kuwa ni bendi gani imetumia kipande hicho cha shairi kukiweka kwenye wimbo wao.

Ni Bima Lee, ambayo walifanya hivyo kwenye wimbo wao wa 'Masimango'. Wao waliimba hivi. "Sheria ya binadamu yataka kujichumia, kwa jasho lako, kila pembe na ujitume, siyo ungoje kuchumiwa, wewe ukae kutumia bwana eee."

Akilimali Snow-White, ndiye mwandishi ambaye vitabu vyake na mashairi yake kwa kiasi kikubwa yamechukuliwa na watunzi na wanamuziki wengi wa zamani na kuyaweka kwenye nyimbo zao.

Kuna shairi lake lingine liitwalo 'Mapenzi Niliyo Nayo', baadhi ya maneno yameandikwa hivi.

"Mchana kutwa nalia, kwa fikirazo benati, Moyo wanichechemea, kwa penzi sili seketi, Mapenzi niliyonayo, kwako hayana kiasi, kwa wingi yamefurika, mapenzi nikupendayo, mwili damu nakauka, haunitulii moyo."

Vipande vya maneno haya, vimewekwa kwenye wimbo wa Super Matimila ya Remmy Ongala, kwenye wimbo wa 'Mariam'.

"Sili nafikiri zaidi kuliko wewe, nakonda kama mnazi kwa mapenzi niliyonayo, moyo wanichechemea, mwili damu nakauka mpenzi ee."

Tukitoka kwa mshairi huyo tunakwenda kwa mshairi na mwandishi maarufu zaidi Afrika Mashariki na Kati, Shaaban Robert. Baadhi ya wanamuziki wamechukua maandishi yake na kuyaweka kwenye nyimbo zao.

Shaaban Dede akiwa na OSS ya Ndekule aliimba wimbo wa 'Nyumba ya Mgumba Haina Matanga'. Maneno mengi ya wimbo ule yametoka kwenye kitabu cha 'Kusadikika' cha Shaaban Robert. Ni mfalme ambaye alikuwa hana mtoto, ana kila kitu, cheo, pesa, hekima na kila kitu, lakini ugumba umevunja heshima yake. Alikuwa akiwaza na kuwaita waganga wote walio kwenye himaya ya utawala wake wamsaidie. Dede naye alichukua baadhi ya maneno na kuyaweka kwenye wimbo wake huo.


"Nimejaliwa elimu iliyonipatia heshima, nina madaraka na uwezo wa kununua chochote duniani, lakini ugumba, umevunja heshima yangu." Ni baadhi ya maneno kwenye wimbo huo, ambayo yamenukuliwa kwenye kitabu hicho.

Juwata Jazz Band wana wimbo uitwao 'Pamela' uliotungwa na Fresh Jumbe. Mtunzi anamwambia mpenzi wake Pamela kuwa kadri itakavyokuwa, wema wake ni la asili, naye kwa vyovyote utakuwa ni la kuiga tu, hivyo hautolingana kamwe.

Mwanaume anarejesha fadhila kwa mpenzi wake, hivyo anamwambia kwa sababu anarejesha huo ni wema wa kuiga, ila ule wa mwanzo wa Pamela ni wa asili.

Vipande vya maneno hayo vinapatikana kwenye kitabu cha marehemu Shaaban Robert, 'Adili na Nduguze.'

**Tuma meseji 0716 350534**



Mwanamuziki mwimbaji, Shaaban Dede, ambaye akiwa na Orchestra Safari Sound','Ndekule', alichukua baadhi ya maneno yaliyokuwa kwenye kitabu cha Shaaban Robert, kiitwacho Kusadikika na kuyaweka kwenye wimbo wake wa 'Nyumba ya Mgumba Haina Matanga.'



Fresh Jumbe ni mmoja wa wanamuziki waliochukua baadhi ya vipande vya maneno kutoka katika kitabu ya Shaaban Robert cha Adili na Nduguze na kupachika kwenye wimbo wa 'Pamela', alioufyatua katikati ya miaka ya 1980 akiwa na Juwata Jazz Band 'Msondo Ngoma.'

HABARI KIMATAIFA

# Marekani yaanza kuilalamikia Israel, yasema imeshindwa kuwalinda raia

**WASHINGTON,** MAREKANI

MAREKANI imeanza kuilalamikia Israel ikieleza mashambulizi inayofanya kusini mwa Ukanda wa gaza hayaendani na maelezo yake ya kuwalinda raia.

Hata hivyo, imeitaka Israel kupunguza idadi ya raia wanaouawa kwa sababu idadi kubwa ya Wapalestina wamepoteza maisha katika operesheni zake zinazoendelea dhidi ya wanamgambo wa Hamas.

Jana Mawaziri wa Mambo ya Nje wa Uingereza Lord Cameron na Marekani Antony Blinken walikutana kwa ajili ya kuzungumzia suala hilo.

Waziri Blinken alivikosoa hadharani vikosi vya Israel jinsi vinavyopigana Ukanda wa Gaza na kukiuka kile walichosema awali kuwa watazingatia kupunguza madhara kwa raia.

"Bado inabakia kuwa muhimu kwa Israeli kuwalinda raia wakati wa vita hivi ," alisisitiza.

Awali Israel ilieleza kuwa inachukua hatua za kupunguza madhara kwa raia, lakini katika siku za hivi karibuni maelfu ya wapalestina wameuawa, ikiwa ni pamoja na maeneo ambayo watu waliambiwa kwenda kwa usalama wao.

Alisema Israel pia inapaswa kusaidia kurahisisha njia ya kufikisha misaada zaidi kwa raia ambao wanakabiliwa na upungufu wa mahitaji muhimu.

Aidha Waziri Blinken alisema kuna pengo kati ya nia ya Israel ya kuwalinda raia na jinsi vita halisi inavyoendelea Ukanda wa Gaza.

"Ni muhimu Israeli kuweka mipango ya kuwalinda kwa kuzingatia kile nilichosema nilipokuwa huko, dhamira ya kuwalinda raia, na matokeo halisi tunayoyaona ni tofauti," alisema Blinken.

Katika hatua nyingine, Israel imekubali kufungua mpaka wa Kerem Shalom kwa ajili ya kukagua bidhaa zinazopelekwaUkanda wa Gaza kutoka nchini Misri.

Marekani imekuwa ikizungumza na Israel kuhusu kutekeleza "usitishaji wa muda wa mapigano kila siku" katika vita na kuwafahamisha Wagaza wanakoweza kwenda ili kuepuka hatari.

"Israel ina wajibu wa kufanya kila linalowezekana katika kuwalinda raia na kuongeza misaada ya kibinadamu," alisema.

Wakati huo huo, Umoja wa Mataifa umeeleza kwamba mpango wa kibinadamu katika Ukanda wa Gaza haufanyi kazi tena.

Mkuu wa Umoja wa Mataifa wa masuala ya kibinadamu Martin Griffiths alisema watu wanaoishi Gaza hawawezi kutoka kuepuka kifo, badala yake hawana matumaini ya siku zijazo.

Alisema dhana halisi ni kuwa hakuna mahali salama maeneo yote ya Gaza na kusababisha kazi ya usambazaji misaada kuwa ngumu.

"Ikiwa unapanga utoaji wa misaada ya kibinadamu kwa Gaza leo, lazima upange uwezekano wa kushambuliwa," alisema.

Akitoa wito wa kusitishwa kwa mapigano, Griffiths alisema kuharibiwa kwa mfumo wa afya wa Gaza kuna hofu ya kuenea kwa magonjwa miongoni mwa raia.

Aidha, Mji wa Khan Younis, ulioko kusini mwa Gaza umekuwa kitovu cha mapigano baada ya jana kushambuliwa kwa mabomu.

Israel ilisema kuwa vikosi vyake vinaendelea kuzingira eneo hilo.

Picha mbalimbali zilizopigwa kutoka mji huo kupitia mashirika ya Habari ya kimataifa, zilionyesha hali ilivyokuwa ya kuhuzunisha ikiwamo matukio ya watu waliojeruhiwa wakipelekwa hospitalini, na wengine wakiwa wamelala kwenye sakafu wakisubiri matibabu.

**BBC**

## Rais Lula aikosoa Ulaya kutobadilika

**BRASILIA, Brazil**

RAIS wa Brazil, Luiz Inacio Lula da Silva ameyakosoa mataifa ya Ulaya kwa tabia yao ya kutobadilika.

Da Silva alisema hayo wakati makubaliano ya kibiashara kati ya Jumuiya ya Ushirikiano wa Umoja wa Ulaya na Amerika ya Kusini yakiwa yamekwama.

Kiongozi huyo alikuwa na matumaini makubaliano hayo yangefikiwa kwenye mkutano wa kilele baina ya Ulaya na Amerika Kusini, baada ya majadiliano yaliyofanyika kwa zaidi ya miaka 20.

Ndani ya makubaliano hayo kunatarajiwa kuanzishwa ukanda huru mkubwa wa kibiashara ulimwenguni.

Umoja wa Ulaya unaitaka Amerika ya Kusini kuhakikisha ikiwa uzalishaji wa bidhaa za kilimo zitakazouzwa nje hautaharibu msitu unaosababisha mvua wa Amazon au mifumo mingine muhimu ya ikolojia.

Rais Lula da Silva alisema Ulaya haitaki kubadilika na kukosoa vikali sera ya kujilinda ya Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macron aliyeyapinga makubaliano hayo walipokutana pembezoni mwa mkutano wa mazingira wa COP28 uliofanyika Dubai.

**DW**



Raia wa Palestina wakimuokoa mtoto baada ya kukwama kwenye kifusi cha nyumba iliyolengwa katika mashambulizi ya mabomu yanayofanywa na vikosi vya Israel kusini mwa Ukanda wa Gaza jana. **PICHA: GETTY IMAGES**

# Sudan Kusini yaondoa kikosi chake DRC

**GOMA,** DRC

KIKOSI cha Jeshi la Sudan Kusini kilichokuwa kikilinda Amani nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) kimeanza kuondoka.

Wanajeshi hao waliondoka jana mashariki mwa DRC kama sehemu ya kikosi cha jumuiya ya Afrika Mashariki (EACRF).

Mapema leo, kikosi cha kwanza cha Sudan Kusini kimeondoka Goma huku kingine kikitarajiwa kuondoka baadae leo.

Jana ilikuwa siku ya mwisho kwa vikosi vya walinda amani kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki kuwepo nchini humo baada ya DRC kukataa kutoa kibali cha kuendelea na majukumu yake.

Vikosi hivyo vilipewa muda wa miezi mitatu ambao uliisha Septemba, lakini viliendelea na kazi yake baada ya kuongezwa mara mbili. Mapema wiki hii majeshi ya Kenya yaliondoka nchini DRC kupitia uwanja wa ndege wa Goma.

Wakuu wa majeshi ya nchi za Afrika Mashariki walikutana mjini Arusha na kuafiki kumaliza shughuli zote kuwa Januari 2024.

DRC ilijiunga na EAC mwaka wa 2022 na mwishoni mwa mwaka huo kikosi cha kijeshi cha jumuiya hiyo kikaingia mashariki mwa taifa hilo kwa ajili ya kulinda amani.

**BBC**

# Guyana, Venezuela wagombea eneo lenye mafuta

**NEW YORK,** MAREKANI

BARAZA la Usalama la Umoja wa Mataifa limepanga kukutana kwa dharura baada ya nchi ya Guyana kuomba kuijadili Venezuela ambayo inataka kupora sehemu ya ardhi yake.

Katika barua kwa rais wa baraza hilo, Waziri wa Mambo ya Nje wa Guyana, Hugh Hilton Todd, ameishutumu Venezuela kwa kukiuka Mkataba wa Umoja wa Mataifa kwa kujaribu kulichukua eneo Essequibo lenye utajiri wa mafuta na madini.

Inadai Venezuela tayari imepanga kupiga kura ya maoni kulichukua eneo hilo. Mvutano juu ya eneo hilo ulianza tangu mwaka 1962 baada ya Venezuela kupinga makubaliano ya mipaka kati ya nchi hizo mwaka 1899.

2015 mvutano uliongezeka baada ya kampuni ya mafuta ya ExxonMobil kutangaza ugunduzi wa kiasi kikubwa cha mafuta katika pwani ya bahari.

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## MAOMBI LA KUONESHA NIA YA KUTOA HUDUMA ZA USIMAMIZI WA MATUKIO YA KISHEREHE KWA AJILI YA KAMPUNI YA EACOP LTD NCHINI TANZANIA - KUMBUKUMBU NA. 00000436

Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) LTD (''EACOP LTD''), inaalika kampuni zenye uzoefu na weledi wa kutosha kuonesha nia ya kutoa Huduma za Usimamizi wa Matukio ya kisherehe katika Mradi wa EACOP nchini Tanzania.

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba la kusafirisha Mafuta lililofukiwa chini ya ardhi linalokatisha mipaka ya nchi mbili litakalo safirisha mafuta ghafi Kwenda katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka rasi ya Chongoleani karibu na Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 296 zitakuwa nchini Uganda na kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:**
Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) LTD inaalika watoa huduma wenye uzoefu na weledi wa kutosha kuonesha nia yao ya kutoa Huduma zifuatazo za Usimamizi wa Matukio ya kisherehe nchini Tanzania.

- Uanzishaji , Uratibu na Usimamizi wa Wazo la Matukio
- Utoaji wa Utaratibu wa Matukio
- Usimamizi wa Uandaji wa Matukio
- Usimamizi wa Upambaji wa Matukio ndani na nje kwa kuzingatia chapa ya kampuni
- Uzoefu wa Masoko

**VIGEZO MUHIMU:**
Makampuni au taasisi zinzoonesha nia zinaalikwa kutuma maombi na kuambatanisha nyaraka zifuatazo:

- Maelezo ya uzoefu, utalaamu na uwezo wa kutoa huduma katika mawanda yanayohitajika
- Wasifu wa Shirika unaoonyesha huduma zinazotolewa, uthibitisho wa utendaji, pampja na barua za uthibitisho kutoka kwa wateja watatu wa awali.
- Leseni ya Biashara
- Cheti cha usajili toka BRELA (ambatanisha kivuli cha cheti)
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Cheti cha Uthibitisho wa Mlipa Kodi kwa mwaka uliopita.
- Waombaji wanasisitizwa sana kuhakikisha kuwa wamesajiliwa kwenye kanzidata ya EWURA (LSSP) ya Watoa Huduma za Ugavi wa Ndani, wakati wa kuwasilisha maombi ya kuonesha nia,
- Kuzingatia Kanuni za Watoa Huduma wa Ndani za mwaka 2017 na ufafanuzi wa Makampuni ya Ndani
- Wasifu wa wafanyakazi muhimu watakaohusika katika mradi, ikiwa ni pamoja na vyeti vyao muhimu, viwango vya elimu, uzoefu , na uwezo wa kutoa huduma zinazohitajika
- Uwezo wa kifedha wa kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kuwasilisha hesabu za fedha za miaka mitatu iliyopita.
- Uthibitisho kutoka kwenye mfumo wa Usimamizi wa QHSE, taasisi na mchakato kulingana na Viwango vya Ndani na vKi-Sekta vinavyotumika kwa kazi zinazofanana na hii.
- Uthibitisho wa kukubaliana na sera za kupinga rushwa, ufisadi, na Haki za Binandamu

Kampuni zenye nia, ambazo zina uwezo na rasilimali za kutosha kutoa huduma zilizotajwa hapo juu zinapaswa kutuma maombi na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe ya **procurement.tz@eacop.com** (ukubwa wa barua pepe usizidi 20Mb) mnamo au kabla ya saa **11:00 jioni** kwa saa za Afrika Mashariki (EAT) mnamo au kabla ya tarehe **23 Disemba 2023**. Kichwa cha Barua pepe kiwe **00000436** - Utoaji wa Huduma za Usimamizi wa Matukio ya Kisherehe. Maombi yote yakuonesha nia yawe kati ya kurasa 10 hadi 20
Maombi yote lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kingereza

**Muhimu:** Kampuni ya EACOP LTD itapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia kulingana na tangazo hili la kuonesha nia na kufanya tathmini kwa kuzingatia vigezo vya ndani ili kubaini kampuni ambazo zitakazojumuishwa kwenye orodha ya makampuni ya awali yenye vigezo. Mwaliko wa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa makampuni ya awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji waTaarifa (NDA). Kampuni ya EACOP LTD inaheshimu haki katika kufanya maamuzi ya kuchagua au kukataa kampuni na kuheshimu maamuzi yake pasipo kutoa sababu kwa kampuni husika.

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## MAOMBI YA KUONESHA NIA YA KUTOA HUDUMA ZA USIMAMIZI WA MAHUSIANO YA UMMA, KIDIJITALI NA VYOMBO VYA HABARI KWA AJILI YA KAMPUNI YA EACOP LTD NCHINI TANZANIA - KUMBUKUMBU NA. 00000435

Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) LTD (''EACOP LTD''), inaalika kampuni zenye uzoefu na weledi wa kutosha kuonesha nia ya kutoa Huduma za Usimamizi wa Mahusiano ya Umma, Kidijitali na Vyombo vya Habari katika Mradi wa EACOP nchini Tanzania.

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba la kusafirisha Mafuta lililofukiwa chini ya ardhi linalokatisha mipaka ya nchi mbili litakalo safirisha mafuta ghafi Kwenda katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka rasi ya Chongoleani karibu na Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 296 zitakuwa nchini Uganda na kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:**
Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) LTD inaalika watoa huduma wenye uzoefu na weledi wa kutosha kuonesha nia yao ya kutoa Huduma zifuatazo za Usimamizi wa Mahusiano ya Umma, Kidijitali na Vyombo vya Habari nchini Tanzania.

- Huduma za usimamizi wa Mahusiano ya umma na vyombo vya habari
- Huduma za usanifu wa kidijitali, ikiwa ni pamoja na utengenezaji wa matangazo ya kidijitali, uwasilishaji wa Habari kwa njia picha, picha mjongeo na maelezo kwa njia vielelezo kwa ajili ya vyombo vya Habari vya kidijitali.
- Huduma za Mipango na Utumiaji wa vyombo vya Habari
- Huduma zitokanazo na vyombo vya Habari

**VIGEZO MUHIMU:**
Makampuni au taasisi zinzoonesha nia zinaalikwa kutuma maombi na kuambatanisha nyaraka zifuatazo:

- Maelezo mafupi ya uzoefu, utaalamu na uwezo wa kutoa huduma katika mawanda husika
- Wasifu wa Shirika unaoonyesha huduma zinazotolewa, uthibitisho wa utendaji, pamoja na barua za uthibitisho kutoka kwa wateja watatu wa awali.
- Leseni ya biashara
- Cheti cha usajili wa Kampuni toka BRELA (ambatanisha nakala)
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Cheti cha Uthibitisho wa Mlipa Kodi kwa mwaka uliopita.
- Waombaji wanasisitizwa sana kuhakikisha kuwa wamesajiliwa kwenye kanzidata ya EWURA (LSSP) ya Watoa Huduma za Ugavi wa Ndani, wakati wa kuwasilisha maombi ya kuonesha nia,
- Kuzingatia Kanuni za Watoa Huduma wa Ndani za mwaka 2017 na ufafanuzi wa Makampuni ya Ndani
- Wasifu wa wafanyakazi muhimu watakaohusika katika mradi, ikiwa ni pamoja na vyeti vyao vya muhimu, viwango vya elimu, uzoefu , na uwezo wa kutoa huduma zinazohitajika.
- Uwezo wa kifedha wa kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kuwasilisha hesabu za fedha za miaka mitatu iliyopita.
- Uthibitisho kutoka kwenye mfumo wa Usimamizi wa QHSE, taasisi na mchakato kulingana na Viwango vya Ndani na Ki-Sekta vinavyotumika kwa kazi zinazofanana na hii.
- Uthibitisho wa kukubaliana na sera za kupinga rushwa, ufisadi, na Haki za Binandamu

Kampuni zenye nia, ambazo zina uwezo na rasilimali za kutosha kutoa huduma zilizotajwa hapo juu zinapaswa kutuma maombi na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe ya **procurement.tz@eacop.com** (ukubwa wa barua pepe usizidi 20Mb) mnamo au kabla ya saa **11:00 jioni** kwa saa za Afrika Mashariki (EAT) mnamo au kabla ya tarehe **23 Disemba 2023**. Kichwa cha Barua pepe kiwe **00000435 -** Utoaji wa Huduma Usimamizi wa Mahusiano ya Umma, Kidijitali na Vyombo vya Habari. Maombi yote yakuonesha nia yawe kati ya kurasa 10 hadi 20.
Maombi yote lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kingereza.

**Muhimu:** Kampuni ya EACOP LTD itapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia kulingana na tangazo hili la kuonesha nia na kufanya tathmini kwa kuzingatia vigezo vya ndani ili kubaini kampuni ambazo zitakazojumuishwa kwenye orodha ya makampuni ya awali yenye vigezo. Mwaliko wa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa makampuni ya awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji waTaarifa (NDA). Kampuni ya EACOP LTD inaheshimu haki katika kufanya maamuzi ya kuchagua au kukataa kampuni na kuheshimu maamuzi yake pasipo kutoa sababu kwa kampuni husika.

# HADITHI

## MAMA MWENYE NYUMBA - 5

MWANTUMU, au mama Mwadawa, ni mwanamke ambaye muda wote yeye anachowaza ni umbea, ugomvi na kufitinisha watu. Anawagombanisha majirani wasielewane, ndoa za majirani zake nazo haziko salama hajaziacha, kwani amekuwa akizitikisa. Kwa bahati mbaya au nzuri anaishi kwenye nyumba ya urithi ya marehemu mama yake, yeye akiwa ndiye mama mwenye nyumba. Cheo hicho cha Umama wa Nyumba asiyojenga, ndiyo akawa amepata fimbo ya kuwapigia watu. Wapangaji wanaopanga kwenye nyumba hiyo wamekuwa wakiishi kwa amri, manyanyaso, kufokewa kama watoto wadogo. Ndani ya nyumba hiyo, wapangaji wamekuwa kama wakiishi bure au kwa mama wa kambo, huku silaha yake kubwa ikiwa ni kuwatishia kuwahamisha. Hebu fuatilia mwanzo na mwisho wa visa vya mama huyu.

**Na Adam Fungamwango : (0716 350534)**




Mama Abdul alipokuwa akiaga tu, Mwantumu akapata mgeni mwingine. Ni Bishada.

Haraka haraka, akajua nini amefuata. Umbea. Akakumbuka siku ile alipokutana naye njiani alimuahidi kumpa maneno.

"Kwanza nilitaka kukufuata nikupe taarifa ya shughuli shoga yangu, miezi miwili ijayo, dada yangu Mkuranga anaozesha, halafu nikupe umbeya.

Huu umbea wako mwenyewe. Wanavyokuongelea. Yaani shoga yangu ukiwa unaongea na watu, ukiwapa kisogo tu, wanakung'ong'a. Wanakuongelea vibaya dada yangu, yaani wewe hapo huna nguo."

Akakumbuka kuwa hakukuwa na umbea wowote, ila ilikuwa ni kupoza joto la kudaiwa taiti, gauni na blauzi.

Hata hivyo hakijaharibika kitu, akajiandaa kutunga uongo. Kumsingizia mtu. Akajiuliza amsingizie nani?

"Karibu shoga yangu Bishada" Akamkaribisha kwenye mkeka.

Mama Mwadawa akaingia ndani. Nia ilikuwa ni kujipa muda kidogo kutunga uongo.

Biashada akasubiri kiasi cha dakika 10 hivi. Mwenyeji wake akatoka nje. Akakaa kwenye mkeka.

"Enhee bibi wewe, nafasi nilikuwa sina wiki yote hii, mara kwenye vikoba, mara hospitali kumuona mgonjwa, sikupata muda. Lakini nilikuwa na kimuhemuhe mwenzangu cha kumjua huyo mbea wangu, enhee nipe ubuyu.

"Huyo mpangaji wangu mmoja wa chumba kile cha mwisho!" Tayari alishatunga uongo.

"Nimemsikia kwa masikio yangu mawili haya hapa."

"Kasemaje?"

"Eeee, bibi wewe, mimi na nakwambia tu, usikurupuke, ukaenda kumwambia, halafu ukasema mimi ndiyo niliekwambia."

"Wala mama Mwadawa!"

"Basi dada, hukuwepo malaika wako alikuwepo."

Bishada alimtumbulia macho kutaka kujua nini aliambiwa.

"Kuna kipindi fulani hivi kama mwezi mmoja uliopita si ulikuwa unaumwa tumbo?"

"Ndiyo, ni kweli..."

"Hapo hapo dada, basi yule mpangaji wangu mama Tausi si akaanza kusambaza umbea kuwa ulikuwa umetoa mimba!"

"Eeee, mimba naitoaje wakati nina mume?" Akahoji.

"Sijui sasa yeye!"

"Mmmh! Makubwa. Haya kama yeye ndiye alikuwa daktari ananitoa sawa!" "Bibi wee, usije ukanitaja. Ujua mimi nakaa na wapangaji ambao hata siwaelewi humu ndani. Ni wagomvi. Halafu wote kama wamezaliwa baba mmoja mama mmoja."

"Haya shoga mimi nimekuja mara moja, nimeacha maharage yangu jikoni, ngoja niwahi yasije yakaungua bure."

"Umepikia kwenye jiko la gesi?"

"Subutu, mkaa, gesi nipikie maharage hiyo pesa ya kujaza nitakuwa naiokota wapi mimi?"

"Basi ngoja nikusindikize, maana na mimi nina safari zangu."

**"Kwanza asitupigie kelele, vichwa vinatuuma, tangu lini akapika huyo, kutwa kiguu na njia kwenda kudowea chakula kwa watu." Huyu sasa alikuwa Devota.**

************************************

"Jamani humu ndani mbona mnanitafuta! Na mtanipata mwaka huu, nani aliyenichukulia mkaa wangu, niliuweka humu kwenye kiroba, naona umepungua, mwanamke gani asiye na adabu huyu? Nataka nirudishiwe mkaa wangu!" Ilikuwa ni sauti kali ya Mama Mwadawa akiwa amerejea kwenye safari zake tangu alipoondoka na Bishada.-

Haikujulikana kama ni kweli, au alikuwa anataka tu ugomvi, maana kila siku ilikuwa lazima amtafute mtu wa kugombana naye ndiyo aone raha.

Wapangaji walikuwa wamechoka na visa vyake, kwa hiyo hawakumuogopa hata chembe. Nao pia walikuwa wamechoka kuishi hapo. Walichokuwa wanasubiria ni kodi zao tu ziishe.

"Bwana eee, umetuchosha, una hela gani wewe ya kununua mkaa?" Sauti ya Tabia ilisikika chumbani kwake.

Tabia tangu siku ile walivyogombana kuhusu kukata kamba ya kuanikia nguo na kumsingizia yeye alikuwa 'anammaindi' na alimuwekea siku yake kuwa kabla hajahama amtie mikononi na kumfumua kisawasawa.

Wakati mama mwenye nyumba anatafuta jibu la kumrudishia Tabia anasikia sauti ya mpangaji wake mwingine ikisema.

"Kwanza asitupigie kelele, vichwa vinatuuma, tangu lini akapika huyo, kutwa kiguu na njia kwenda kudowea chakula kwa watu." Huyu sasa alikuwa Devota.

Nia yangu wagombane na mama mwenye nyumba kwenye zamu ya kufagia, na kumchamba kuhusu nyumba, ilikuwa kama wanawindana hivi.

"Ahaa, nyinyi ndiyo mmenichukulia mkaa wangu, nautaka, la sivyo mtaona leo timbwili la Asha Ngedele leo. Nitaingia kwenye chumba cha mmoja baadaye mwingine..." Akakatishwa na sauti ya Tabia.

"Cha nani, ingia kama mwanamke kweli, ingia nikufinyange kama unga wa ngano. Na nilivyokuwa na hasira na wewe."

"Mimi nimepumzika na mume wangu, haya fungua huo mlango utuone tulivyolala kama inakuhusu."

"Nasema hivi nimewachoka wapangaji wote nyinyi, kodi zenu zikiisha muhame..." Mwantumu alipiga kelele kwa hasira baada ya kuona kila siku anakosa heshima na udhibiti wa heshima ya mama mwenye nyumba.

Wapangaji wake walionekana kumdharau na kumjibu kila wanachojisikia kujibu.

Kwa ile sauti alivyoipandisha, Devota na Tabia waliangua vicheko kila mmoja chumbani mwake kama wameambizana vile.

"Tunasubiri kodi iishe tu dada, nani anataka tena kukaa kwenye kijumba chako hiki kibovu na mvua hizi. TV yangu imeingia maji nimekwenda kuitengeneza, shilingi elfu ishirini zimenitoka, mwenyewe nimezipatia tabu nimetoka kudanga huko, narudi nakuta nyumba yote inavuja, TV kila nikiwasha wapi. Pesa ya kudanga ikabidi nimpelekee fundi inahusu." Bado Tabia alizidi kupiga kwenye mshono.

Wakati huo mama mwenye nyumba akaona ameuwasha moto na hawezi kuuzima, wapangaji wamemchachamalia. Akaamua kuingia ndani kimya kwa hasira. Akaazimia kuwa kesho atakwenda kumuona dalali aanze mipango ya kusaka wapangaji wengine baada ya waliopo kumaliza mikataba yao.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# KIVUMBI NGAO YA JAMII LEO

Na Saada Akida

LEO ni kivumbi katika uwanja wa Azam Complex, Chamazi ambapo macho na masikio ya wapenzi wa soka la wanawake watayaelekeza huko kwenye michezo ya fainali ya Ngao ya Jamii inayoanza leo.

Michuano hiyo inayofanyika kwa mara ya kwanza itahusisha timu nne ambazo ni mabingwa watetezi wa Ligi ya wanawake, JKT watakaoumana na Fountain Gate Princess mchezo utakaoanza 9:00 alasiri na baadae mchezo mwingine utawakutanisha watani wa jadi, Simba Queens dhidi ya Yanga Princes, saa 12:00 jioni.

Katika michezo ya leo kuna timu zinahitaji kutafuta heshima na nyingine zikipanga kulipa kisasi au kuendeleza furaha za kaka zao ambao ni Simba Queens dhidi ya Yanga Princess.

Mshindi katika kila mchezo watacheza fainali ya michuano hiyo bna timu nyingine mbili zitacheza kusaka nafasi ya tatu.

Akizungumzia mchezo wake, Kocha Msaidizi wa Simba, Mussa Hassan 'Mgosi', alisema wanamshukuru Mungu na kuwapongeza TFF kwa kuhakikisha soka la wanawake linazidi kukuwa.

Alisema katika maandalizi wamejipanga kwa ajili ya kufanya vizuri katika mchezo wao dhidi ya Yanga Princess kwa kutaka kupata ushindi katika mchezo huu ambao utakuwa sehemu ya maandalizi ya msimu mpya.

"Mechi haitakuwa rahisi kwa sababu timu zote zimejiandaa vizuri, tulikaa na kujiuliza tulipokosea msimu uliopita na tumeona mapungufu yetu na sasa tunataka kufanya vizuri msimu huu na kurejesha furaha ya mashabiki wetu," alisema Mgosi na kuongeza,

"Tunaimani ya kufanya vizuri kwa sababu ya maboresho ya benchi letu la ufundi pamoja na usajili mkubwa tulioufanya katika kuboresha kikosi chetu, tunatarajia msimu huu heshima ya Simba inarejea," alisema Mgosi.

Kwa upande wake, Kocha Mkuu wa Yanga Princess, Charles Haalubono, alisema wamejiandaa vizuri kukabiliana na Simba Queens ambao anaamini ni timu ngumu lakini kikosi chake kipo tayari kwa mchezo.

"Itakuwa mechi ya ushindani natambua ni mechi kubwa na ni dabi, lakini tumejipanga vizuri na tunatambua katika historia hatuna matokeo mazuri, hatutaki kuamini hayo kwa sababu wachezaji wangu wako tayari kwa ajili ya kutafuta matokeo mazuri," alisema Haalubono.


Kocha wa JKT Queens, Esther Chabruma kwa upande wake alisema maandalizi kwa upande wake yanaendelea vizuri kikubwa wachezaji wako katika hali nzuri kwa ajili ya mchezo wao dhidi ya Fountain Gate Princess.

"Hatutakuwa na mabadiliko yoyote katika kikosi changu cha ushindani, nitawakosa nyota wangu wawili, katika mchezo hakuna kujiamini sana kwa sababu wachezaji wangu wengi walikuwa kwenye majukumu ya timu ya Taifa na tutapambana kupata matokeo mazuri," alisema Chabruma.

Aliongeza kuwa licha ya kutokuwepo kwa baadhi ya wachezaji wake lakini anaimani waliopo ndani ya kikosi hicho wanaweza kufanya vizuri na kuwapa ushindi.

Aidha, kocha wa Fountain Gate Princess, Masuod Juma alisema wapo tayari kukabiliana na wapinzani wao na kikubwa wanataka kuchukua ubingwa huo mwaka huu.

"Tunajua ubora wa JKT Queens, mechi ya mwisho walitufunga lakini sasa tumeimarika zaidi, tutacheza kwa nidhamu kubwakwa sababu wapinzani wetu ni timu bora, lengo niushindi tu," alisema.




Msemaji wa kampeni ya 'magift dabo' Haji Manara (kulia) akimkabidhi mfano wa hundi ya shilingi milioni moja, mmoja wa washindi wa wiki ya pili wa shindano hilo, Emmanuel Mboya wa Bagamoyo jana jijini Dar es Salaam. **PICHA:MPIGAPICHA WETU**

# Washindi 13 'Magift dabo' wapatikana

Na Mwandishi Wetu

JUMLA ya washindi 13 wamepatikana na kukabidhiwa zawadi zao katika wiki ya pili ya kampeni ya magift dabodabo inayoendeshwa na kampuni ya Tigo.

Akizungumza wakati wa kuwakabidhi zawadi zao, Msemaji wakampeni hiyo, Haji Manara, alisema kuwa kampeni hiyo ndio kwanza imeanza na kuwataka wananchi wengi kushiriki kuweza kujiweka katika nafasi ya kushinda zawadi kwenye msimu huu wa sikukuu.

"Tunaendelea kuwahimiza wateja wa Tigo kuendelea kutumia huduma za tigopesa kuweza kushinda, kampeni hii haidanganyi, ukishinda mara moja unakabidhiwa zawadi yako," alisema Manara.

Alisema walioshinda zawadi kwa wiki hii ya pili ni washindi 13 kutoka maeneo tofauti tofauti.

"tuna wasindi wa pesa kuanzia shilingi milioni moja mpaka milioni 10, washindi wa vifaa vya umeme vya majumbani na wengine wa safari ya kwenda Zanzibar,"alisema manara.

Aliwataja baadhi ya washindi hao kuwa ni pamoja na Mama lishe, Rehema Makunganya wa Mbezi Kimara-Dar es Salaam aliyeshinda Shilingi milioni 10, Abul Kilabula wa Chanika aliyejishindia vifaa vya umeme vya majumbani ambavyo ni friji, televisheni, radio ya kisasa na kifaa cha kupashia moto vyakula.

Washindi wengine ni mfanyabiashara wa ubuyu Mkoani Dodoma, Janeth Kamili aliyeshinda Shilingi milioni moja, Asma Kiongozi, mwanafunzi mkoani Iringa ambaye naye ameshinda kiasi hicho cha fedha.

Mmoja wa washindi hao, Kilabula, aliwashukuru Tigo kwa kuendesha kampeni hiyo na kuwataka watu wengine watumie zaidi huduma za tigopesa kuweza kushinda.

"Mwanzoni mimi sikuamini kama mtu anaweza kushinda kweli, lakini leo (jana) nimekuwa shahidi kuwa ni kweli, watu washiriki waweze kushinda kama mimi, nimeshinda vifaa hivi na nimemchagua mtu nimpendaye naye ashinde, nimemchagua mke wangu na yeye kashinda," alisema Kilabula mkazi wa Chanika.

## Wavu Dar watembeza bakuli

Na Moshi Lusonzo

CHAMA cha Mpira wa wavu Mkoa wa Dar es Salaam (DAREVA) kimewaomba wadau wa michezo kujitokeza kuzichangia timu zake zitakazoshiriki michuano ya kombe la taifa itakayofanyika jijini Dodoma.

Mashindano hayo yatakayoshirisha timu za mikoa yote ya Tanzania bara yanatarajiwa kuanza kutimua vumbi kuanzia Desemba 18 hadi 23 mwaka huu.

Mwenyekiti wa DAREVA, Fred Mshangama, alisema timu mbili zitashiriki katika mashindano hayo ambazo ni za wanaume na wanawake zote kwa pamoja zikiwa na wachezaji 30 na wanahitaji fedha za maandalizi pamoja na vifaa muhimu.

Amewaomba wadau wa michezo kuguswa na ushiriki wa timu hizo kwa kuichangia kwa hali na mali.

**Alisema, kutokana na umuhimu wa Mashindano hayo, wa nahitaji kujiandaa kwa ukubwa wake, hivyo wanahitaji kuji tosheleza kwa vifaa na mahitaji mengine.**

" Tunaendelea kuiandaa timu kwa ajili ya Mashindano haya, tunachohitaji katika kipindi hiki ni fedha na vifaa ili timu zote mbili ziende Dodoma zikiwa na mahitaji yote muhimu," alisema

Aidha, Mshangama aliwataka wafadhili na wadau hao kuwekeza katika mpira wa wavu kwani una mashabiki wengi kuanzia ngazi za shule za msingi, Sekondari mpaka vyuoni.

## ZISIKUPITE

**NYOTA KUUZWA MAN UNITED**
MANCHESTER United iko tayari kusikiliza ofa kwa kiungo wa kati wa Brazil, Casemiro mwenye umri wa miaka 31, mlinzi wa Ufaransa Raphael Varane mwenye miaka 30, na winga wa England, Jadon Sancho mwenye miaka 23, huku kocha Erik ten Hag akijaribu kupunguza kikosi chake. (***Independent***)

**BRANTHWAITE ATAKIWA SPURS**
MLINZI wa kati wa Everton, Jarrad Branthwaite mwenye umri wa miaka 21 na mlinzi wa Crystal Palace, Marc Guehi mwenye miaka 23 wako kwenye orodha ya wanaosakwa na Ange Postecoglou huku kocha huyo wa Tottenham Hotspur akipanga kuunda upya kikosi cha klabu hiyo. (***Sky Sports***)

**DELE KUREJEA**
KIUNGO wa kati wa Everton, Dele Alli mwenye umri wa miaka 27 anakaribia kurejea kwenye mazoezi kamili huku akiongeza ahueni ya jeraha la paja ambalo limemaanisha kuwa bado hajacheza msimu huu. (***Times***)

**ANDRE ALENGWA**
KLABU ya Fulham itamlenga kiungo wa kati wa Brazil, Andre mwenye umri wa miaka 22, kutoka klabu ya Fluminense iwapo Joao Palhinha mwenye umri wa miaka 28, ataondoka hapo Craven Cottage Januari. (***Telegraph***)

**PALHINHA ATAKIWA ARSENAL**
KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta anataka kumsajili Joao Palhinha kutoka Fulham hatua ambayo itakuwa muda wa mwisho wa kiungo wa kati wa Ghana, Thomas Partey mwenye umri wa miaka 28 kuwa na washikabunduki hao. (***Mirror***)

**GUIRASSYA AKARIBIA MAN**
KLABU ya Manchester United na Newcastle United sasa zinaongoza katika kinyang'anyiro cha kumsajili mshambuliaji wa Guinea, Serhou Guirassy mwenye umri wa miaka 27 kutoka Stuttgart. (***Football Insider***)

**RABIOT KUSUSIA**
KIUNGO wa kati wa Ufaransa, Adrien Rabiot mwenye umri wa miaka 28 atasusia kuhamia Ligi Kuu ya England na kutia saini mkataba mpya na Juventus. (***Gazzetta Dello Sport***)

**MARTINEZ MKATABA MPYA**
KLABU ya Inter Milan imepanga kuvunja mfumo wao wa mishahara ili kumsainisha mshambuliaji wa Argentina, Lautaro Martinez mwenye umri wa miaka 26 kwenye mkataba mpya wa muda mrefu. (***Calciomercato***)

**CHERKI KUUZWA JANUARI**
KLABU ya Lyon iko tayari kumuuza mshambuliaji wa Ufaransa, Rayan Cherki mwenye umri wa miaka 20 Januari huku West Ham na Chelsea wakimtaka. (***Footmercato***)

**WERNER ANAWEZA KUONDOKA**
FOWADI wa Ujerumani, Timo Werner ameambiwa na Mkurugenzi wa michezo wa RB Leipzig, Rouven Schroder kwamba anaweza kuondoka katika klabu hiyo ya Bundesliga kwa mkopo Januari, lakini si Manchester United wala Real Madrid wenye uwezo wa kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27. (***Bild***)

**TORRES HATAKI KUONDOKA BARCA**
FOWADI wa Hispania, Ferran Torres mwenye umri wa miaka 23 amemwambia kocha wa Barcelona, Xavi kwamba amejitolea kuitumikia klabu hiyo na hataki kuondoka Januari. (***Mundo Deportivo***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# SON AWABWATUKIA WACHEZAJI TOTTENHAM

**●●● Asema wamekuwa laini baada ya kupokea kichapo juzi na sasa wanapaswa....**

**LONDON,** England

MSHAMBULIAJI Son Heung-Min amesema Tottenham Hotspur ni "laini" baada ya kupokea kichapo cha mabao 2-1 kutoka kwa West Ham wakiwa na uongozi wa mapema, na kuwa timu ya kwanza katika historia ya Ligi Kuu England kupoteza pointi wakati ikiwa kwenye nafasi ya ushindi katika mechi tano mfululizo.

Spurs walichukua uongozi wa mapema kupitia kwa bao la Cristian Romero kwa kichwa dakika ya 11 lakini walishindwa kutumia nafasi walizozipata kipindi cha kwanza, huku West Ham wakifunga mabao mawili ya kushambulia katika kipindi cha pili kupitia kwa Jarrod Bowen na James Ward-Prowse.

**"Tulipoteza mchezo ambao haukubaliki," alisema Son akiiambia Amazon Prime katika mahojiano yake baada ya mechi.**

"Unapata bao la kuongoza katika mechi tano mfululizo na kupoteza mchezo, nadhani ni jambo lisilokubalika na kama wachezaji tunapaswa kuwajibika.

"West Ham siku zote imekuwa ngumu kucheza dhidi yao, lakini tazama tulikuwa laini. Hasa katika Ligi Kuu, hata kama unashinda 2-0, 3-0, hujui nini kitatokea mwishoni."

Alipoulizwa iwapo kama hilo linaweza kuwa tatizo la kisaikolojia, Son alijibu: "Hapana. Lakini kama nilivyosema hapo awali wachezaji wanapaswa kuwajibika, na mashabiki hawastahili hili. Unapoongoza 1-0 mapema inapaswa kuleta nguvu zaidi. Hatukufanya hivyo na ndiyo maana tulipoteza."

Matokeo hayo yamekuwa mara ya kwanza tangu mwaka 2008 kwa Spurs kupoteza mechi tatu mfululizo za nyumbani.

Kocha, Ange Postecoglou alisema ni lazima timu yake ianze kusaka matokeo na kuweka wazi inalenga zaidi kushinda kuliko kucheza soka la kufurahisha.

"Ni mchezo mwingine ambapo tulitawala na hatukugeuza hilo kuwa kitu zaidi... tuna safari ndefu kama timu," alisema Postecoglou akiwaambia waandishi wa habari baada ya mechi.

"Sisi kuwa wazuri ina maana tutakuwa mbele kwa mabao 3-0. Hii sio juu ya kucheza mpira mzuri, hii ni kushinda michezo ya mpira wa miguu.

"Nilisema hivyo tangu mwanzo kwamba ninatamani kuunda timu za kushinda michezo. Kuwa 1-0 hadi mapumziko haikuwa mchezo mzuri kwetu, tulipaswa kuwa tatu, au nne bila kumaliza kipindi cha kwanza.

"Nadhani kwa sasa tunapitia kipindi hiki ambapo tunaitwa kucheza mpira mzuri lakini sioni hilo," aliongeza.

Matokeo hayo yanamaanisha Tottenham imebakia nafasi ya tano kwenye msimamo ikiwa na 27 baada ya kucheza mechi 15.

# SUAREZ MCHEZAJI BORA LIGI KUU YA BRAZIL



**RIO DE JANEIRO,** Brazil

MSHAMBULIAJI wa Uruguay, Luis Suárez alishinda Mpira wa Dhahabu siku ya Alhamisi kama mchezaji bora wa msimu katika ligi Kuu ya Brazil (Serie A) kabla ya kuondoka kwake katika klabu ya Gremio.

Suarez mwenye umri wa miaka 37, ambaye alicheza na Lionel Messi kule Barcelona baada ya misimu kadhaa kuwa na Liverpool na Ajax, alifunga mabao 17 kama mshindi wa pili wa ligi ya Brazil, Gremio.

Msimu ulimalizika Jumatano kwa Palmeiras kutetea taji lake na Santos kushushwa kutoka ligi kuu kwa mara ya kwanza katika historia ya klabu hiyo.

Suárez alifunga mabao mawili siku ya mwisho ya msimu katika ushindi wa 3-2 dhidi ya Fluminense kwenye Uwanja wa Maracana mjini Rio de Janeiro.

Mfungaji bora wa ligi ya Brazil alikuwa fowadi wa Atletico Mineiro, Paulinho mwenye mabao 20.

Suárez alisema mara nyingi alihofia hangeweza kumaliza msimu nchini Brazil kwa sababu ya maumivu makali ya goti na shida ya safari ndefu za ndege, lakini waandishi wa habari walimpigia kura kushinda tuzo ya Mpira wa Dhahabu.

Suárez aliichezea Gremio mechi 53 na kufunga mabao 26 katika mashindano matatu msimu huu.

"Ninakaribia umri wa miaka 37, huu ndio mwaka ambao nilicheza mara nyingi zaidi katika uchezaji wangu. Pia ulikuwa mwaka ambao mara nyingi nilikuwa mbali na familia yangu. Tuzo hii ni yao," alisema Suárez akitokwa na machozi baada ya kupokea tuzo hiyo kutoka kwa mchezaji mwenzake wa zamani wa Uruguay, Diego Lugano.

Alipoulizwa kuhusu mustakabali wake, Suárez hakujibu, lakini vyanzo vya ESPN vimesema kwamba mpango wake ni kuhamia Ligi Kuu ya Marekani, MLS, katika Klabu ya Inter Miami CF kucheza na tena na Messi umekubaliwa.

Suárez alisema atakumbuka sio tu mashabiki wa Gremio, lakini pia wale wa klabu nyingine vilivyomheshimu kama mpinzani.

"Ni vigumu kuona mashabiki wa wapinzani hapa wakikupongeza unapocheza, na hilo lilinitokea katika baadhi ya maeneo," alisema Suárez.

# Felix amtaka Szoboszlai Barcelona

**BARCELONA,** Hispania

JOAO Felix amefichua kuwa anataka kucheza na nyota wa Liverpool, Dominik Szoboszlai katika klabu ya Barcelona siku zijazo.

Szoboszlai alijiunga na Liverpool kutoka RB Leipzig wakati wa uhamisho wa majira ya joto wa mwaka 2023 kwa pauni milioni 60, akisaini mkataba wa miaka mitano hapo Anfield, na mara moja amekuwa kipenzi cha mashabiki.

Kiungo huyo ameanza mechi zote 14 za Ligi Kuu England akiwa na Liverpool hadi sasa msimu huu, akifunga bao moja.

Kiwango cha Szoboszlai pia kimevutia umakini wa Felix anayecheza kwa mkopo Barcelona pia.

Akizungumza na Spiler TV, Felix alimchagua raia huyo wa Hungary kama mchezaji ambaye angependa kuona akijiunga na Barca siku moja.


"Dominik Szoboszlai wa Liverpool. Napenda mchezo wake, nadhani anaweza kucheza hapa siku moja," alisema.

Felix kwa sasa yuko kwa mkopo Barca kutoka Atletico Madrid na amekuwa kwenye kiwango cha kuvutia katika wiki za hivi karibuni.

Fowadi huyo alikuwa kinara wa mchezo dhidi ya klabu yake mama ya Atleti wikendi uliyopita, akifunga bao pekee katika ushindi muhimu wa LaLiga.

Akizungumza na RAC1, Mkurugenzi wa michezo wa Barcelona, Deco alifichua nia ya klabu hiyo kumsajili Felix kwa mkataba wa kudumu wakati wa dirisha la majira ya joto 2024:

"Ni mapema. Lakini bila shaka tayari tunalifikiria hilo. Tunaona jinsi msimu unavyokwenda."




# Villa yataja dau la Douglas

**LONDON,** England

KLABU ya Aston Villa imeweka wazi kwamba, inahitaji angalau pauni milioni 60 katika dirisha lijalo la majira ya baridi ili kumuuza kiungo wao Mbrazili Douglas Luiz.

Timu nyingi za Ligi Kuu England zimekuwa zikimtolea macho mchezaji huyo, huku Arsenal ikiongoza kwenye mbio za kuwania saini yake.

Vilevile klabu hiyo ya Villa Park imepanga kufanya naye mazungumzo ili kumsainisha mkataba mpya ambao utawekwa kipengele cha pauni milioni 110 kwa timu zitakazohitaji kumnunua.

Mchezaji huyo mkataba wake wa sasa unamalizika mwaka 2026.

Arsenal ndio inadaiwa kuhitaji zaidi huduma ya mchezaji huyo ili azibe pengo la Thomas Partey anayedaiwa kuwa ataondoka Januari au mwisho wa msimu huu.

Inaelezwa kuwa kocha Mikel Arteta ni shabiki mkubwa wa Luiz na ndio amempendekeza akawe mbadala wa Partey.

Luiz ambaye pia anahusishwa na Liverpool, msimu uliopita alicheza mechi 22 za michuano yote na kufunga mabao sita na kutoa asisti nne.

HABARI MICHEZO

# WADAU WAITWA KUZIBEBA STARS, TWIGA STARS AFCON

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI inawaomba wadau wote wa michezo nchini kujitokeza kusaidia kusaka fedha za maandalizi ya Timu za Soka za Taifa (Taifa Stars na Twiga Stars), ambazo zimefuzu kucheza fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON na WAFCON), zitakazofanyika mapema mwakani, imeelezwa.

Akizungumza katika ufunguzi wa Mkutano Mkuu wa 10 wa Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB), Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro, alisema timu hizo zinahitaji kiasi kikubwa cha fedha ili kujiandaa vyema kushiriki fainali hizo.

Ndumbaro alisema serikali na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), pekee hawatamudu kugharamia maandalizi ya timu hizo mbili ambazo zinakwenda katika fainali za Afrika kwa mara ya tatu.

Waziri huyo alisema ili kupata fedha hizo, wizara yake imeandaa harambee itakayofanyika kati ya Januari 2 na 5, mwakani na wadau wakubwa watakaoalikwa kukusanya fedha hizo ni klabu zote za hapa nchini.

"Hapo ndio tutajua nani mkubwa, kama klabu yako kubwa basi utachangia kiasi kikubwa cha fedha, tunaomba mtakapopokea barua za mwaliko mfike bila kukosa, " alisema Ndumbaro.

Bosi huyo wa michezo aliitaka bodi pia kuendelea kuisimamia vyema Ligi Kuu Tanzania Bara na anaamini inaweza kupanda viwango kutoka namba tano hadi namba moja barani Afrika.

"Hili linawezekana, na niliwahi kuelezwa na mtayarishaji mkubwa wa vipindi vya soka kutoka England kuwa dabi ya Yanga na Simba ndio dabi kubwa duniani, tuendelee kuipa thamani na naiomba bodi iendelee 'kuibrand' dabi yetu," Ndumbaro alisema.

Aliongeza katika kuhakikisha Tanzania inaendelea kufanya vyema kwenye mashindano mbalimbali, kila timu ya ligi kuu inatakiwa iwe na timu za vijana na wanawake na akapendekeza kuanzia msimu ujao timu isipotimiza vigezo hivyo isipewe leseni.

Alisema wizara imetenga sekondari 52 ambazo zitakuwa maalumu kwa ajili ya michezo na kuzitaka klabu kwenda kuchagua sekondari moja ambayo itaisimamia na ndiyo rasmi itakuwa timu yao ya vijana.

"Klabu itapeleka makocha wake hapo, itawasimamia ili kuwaendeleza. Tusipofanya hivyo hatutafika kokote," alisema Ndumbaro.

Aliongeza pia kuanzia mwakani timu zote zinatakiwa kuwakatia bima wachezaji wake kwa sababu hii itasaidia kuwaweka salama nyota hao ambao kazi wanayofanya ina hatari ya kuumia.

Naye Mwenyekiti wa TPLB, Steven Mguto, aliipongeza Yanga kwa kufika fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika msimu uliopita sambamba na Simba kucheza hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Mguto alisema pia anazitakia heri na mafanikio Simba na Yanga ambazo zote msimu huu zimetinga hatua ya makundi ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika ambayo bado inaendelea.

Mwenyekiti huyo alikemea vitendo vya mashabiki wa hapa nyumbani kuwapa msaada na ushirikiano wa karibu timu ngeni zinapokuja kupambana na kusema jambo hilo linakera na halina afya ya maendeleo ya soka nchini.

Aliishukuru Benki ya Biashara Tanzania (NBC), kwa kuendelea kudhamini Ligi Kuu Bara na Ligi ya Championship lakini ameweka wazi bado timu zina changamoto ya kufikia sifa za kupata leseni ya klabu.



Straika wa Timu ya Soka ya Taifa ya vijana ya umri chini ya miaka 18, Bakari Msimu (kulia), akijiandaa kumtoka nyota wa Rwanda katika mechi ya kusaka mshindi wa tatu kwenye mashindano ya CECAFA U-18 iliyochezwa Kisumu, Kenya jana. Tanzania ilishinda mabao 3-1. **PICHA: TFF**

# Dabo afurahishwa na ubora Azam FC

**Na Saada Akida**

BAADA ya timu yake kupata ushindi mnono wa mabao 5-0 katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya KMC, Kocha Mkuu wa Azam FC, Youssoupha Dabo, amesema hajashangazwa na matokeo waliyopata na hiyo imetokana na ubora wa kikosi chake.

Ushindi huo umeifanya Azam FC kupanda kileleni katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kufikisha pointi 25 baada ya kushuka uwanjani mara 11, ikishinda michezo nane sare moja na kupoteza mchezo mmoja.

Nafasi ya pili katika msimamo huo inashikiliwa na Yanga yenye pointi 24 lakini imecheza michezo tisa huku Simba iliyoshuka dimbani mara nane inafuatia ikiwa na pointi 19.

Akizungumza na Nipashe baada ya kumalizika kwa mchezo huo wa juzi, Dabo, alisema amefurahishwa na kiwango kizuri kilichoonyeshwa na wachezaji wake ingawa haikuwa kazi rahisi kupata ushindi mkubwa na kutoruhusu nyavu zao kutikiswa.

"Sio jambo la kushangaza kwa sababu ya ubora tulionao, na tunataka kuendeleza ubora huu, mipango yangu ni kupambana kwa nguvu kwa sababu ni mwanzo wetu wa kupata ushindi wa namna hii.

Tunahitaji kuongeza umakini kwa sababu unapopata ushindi wa namna hii , tunapaswa pia kusahau yaliyopita, sasa tunaangalia mchezo ujao utakaochezwa Jumatatu dhidi ya JKT Tanzania," alisema Dabo.

Naye Kocha Mkuu wa KMC, Abdihamid Moallin, alisema ulikuwa mchezo mzuri na timu yake ilijaribu kumiliki mchezo lakini Azam walikuwa bora upande wa pembeni unaoongozwa na Kipre Junior pamoja na Gibril Sillah.

Moallin alisema pamoja na matokeo hayo mabaya, wachezaji wake wameendelea kujifunza na kuongeza uzoefu dhidi ya timu ngumu na ataenda kufanyia kazi mapungufu kwa ajili ya kusaka pointi kwenye mechi zinazofuata.

"Kila unapopoteza unajifunza, hivyo kuna funzo tumepata, tunarudi nalo nyumbani tunaendelea kuimarika najua tuna timu nzuri kwenye mbio hizi za Ligi Kuu Tanzania Bara," alisema Moallin.

Ligi hiyo itaendelea tena leo kwa Coastal Union kuwakaribisha Mtibwa Sugar kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani, jijini Tanga.

# Fei Toto: Sifikirii 'kiatu' Bara

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO mshambuliaji wa Azam FC, Feisal Salum 'Fei Toto' ambaye juzi amefikisha mabao saba katika Ligi Kuu Tanzania Bara, amesema lengo lake si kushindana kuwania kiatu cha dhahabu lakini anataka kuisaidia timu yake ifanye vyema msimu huu.

Fei Toto amelingana idadi hiyo ya mabao na wachezaji wa Yanga, Stephane Aziz Ki na Maxi Nzengeli pamoja na Mkongomani Jean Baleke wa Simba.

Mzanzibari huyo ambaye alitua Azam FC akitokea Yanga, aliliambia gazeti hili amejipanga kupambana ili kufunga mabao mengi zaidi msimu huu ambapo juzi usiku iliwachapa KMC mabao 5-0.

"Malengo yangu ni kuipambania timu yangu sio kitu kingine, mengine yatajulikana huko huko mbele ya safari," alisema Feisal ambaye mpaka sasa amehusika na mabao 11, akiwa ametoa pasi nne za mabao.

Alisema siri ya kuendelea kuwa katika kiwango cha juu tofauti na ilivyotarajiwa ni kujituma na kuthamini kipaji chake alichopewa na Mwenyezi Mungu.

"Mimi najisikia vizuri sana, mimi mpira ni kazi yangu, nikienda popote pale na siri ya kuendelea kufanya vizuri ni kujituma, kuheshimu kipaji na kufuata maelekezo ya walimu, kwa sababu ukifanya vyote hivyo uwezo wako unazidi kuongezeka," alisema Fei Toto.

Alisema hana nia ya kuwania tuzo yoyote msimu huu kwa sababu muhimu kwake ni mafanikio ya timu.



# Michezo

Jumamosi Desemba 9, 2023
Nipashe

UK. 21



Son awabwatukia wachezaji Tottenham




Mshambuliaji wa Yanga, Kennedy Musonda (kulia) akiwania mpira na beki wa Medeama kwenye mchezo wao wa kundi D wa Ligi ya Mabingwa Afrika jana kwenye uwanja wa Baba Yaro nchini Ghana. Timu hizo zilifungana bao 1-1. **PICHA: MTANDAO**

# Yanga yajiweka pagumu ligi ya Mabingwa Afrika

## ●●● Sare yawaongezea mlima kufuzu robo fainali, ingawa...

**Na Adam Fungamwango**

YANGA jana iliendelea kujiweka kwenye mazingira magumu ya kufuzu hatua ya robo fainali ya Ligi ya mabingwa Afrika baada ya kulazimishwa sare ya bao 1-1 na Medeama kwenye mchezo wa kundi D uliochezwa kwenye uwanja wa Baba Yaro katika mji wa Kumasi nchini Ghana.

**Matokeo ya jana ya naifanya Yanga kufikisha pointi mbili baada ya kucheza michezo mitatu na kuendelea kuburuza mkia kwenye kundi hilo linaloongozwa na Al Ahly yenye pointi tano baada na wao jana wakiwa nyumbani kulazimishwa suluhu na CR Belouizdad ya Algeria.**

Katika msimamo wa kundi hilo, Belouizdad na Medeama wamefikisha pointi nne mbili zaidi ya Yanga huku zote zikiwa zimecheza michezo matatu.

Ili angalau kufufua matumaini ya kusonga mbele, Yanga sasa wanatakiwa kushinda mchezo wao wa marudiano dhidi ya Medeama utakaochezwa Desemba 20 kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa huku pia wakiombea Al Ahly ishinde mchezo wao wa marudiano nyumbani kwa CR Belouizdad.

Katika mchezo wa jana, kiungo mshambuliaji wa Yanga raia wa Ivory Coast, Pacome Zouzoua kwa mara nyingine tena aliiokoa timu yake isipate kipigo kingine cha ugenini kwenye kundi lao alipofunga bao la kusawazisha katika dakika ya 35 wakati timu yake ikiwa nyuma kwa bao la dakika ya 27 lililofungwa na Jonathan Sowah kwa mkwaju wa penalti iliyotokana na beki Dickson Job kumuangusha kwenye eneo la hatari Derrick Lomotey aliyekuwa akienda kumuona golikipa wa Yanga Djigui Diarra.

Hii ni mara ya pili kwa Pacome kuinusuru timu yake kupata kipigo kwenye michuano hiyo kwani wiki iliyopita kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa aliisawazishia Yanga bao dakika ya 89 dhidi ya Al Ahly ya Misri na kuifanya mechi hiyo kuisha kwa bao 1-1.

Jana Pacome alifunga bao hilo kwa juhudi binafsi baada ya kumpokonya mpira mchezaji wa Medeama katikati ya uwanja na kukimbia nao mpaka ndani ya eneo la hatari na kuachia shuti la chini chini lilomshinda kipa wa Medeama Felix Kyei.

Mpaka timu hizo zinaenda mapumziko zilikuwa zimefungana bao 1-1. Kipindi cha pili kilianza kwa kasi na dakika chache baadae kocha wa Yanga, Miguel Gamondi alifanya mabadiliko kwa kumtoa Clement Mzize na Kennedy Musonda na nafasi zao kuchukuliwa na Aziz Ki na Hafiz Konkoni mabadiliko ambayo yaliimarisha Yanga ambao waliendelea kufanya mashambulizi mfululizo lakini umakini mdogo uliwanyima nafasi ya kuongeza mabao.

Hata hivyo Yanga watapaswa kujilaumu wenye kwa kushindwa kuibuka na ushindi licha ya nafasi nyingi walizozitengeneza hasa kipindi cha pili cha mchezo huo.

Kwa matokeo hayo, bado Yanga inabaki na rekodi ya kutoshinda mechi yoyote ya Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi, si msimu huu tu, bali tangu mfumo huo uanzishwe mwaka 1998 ambapo ilicheza hatua hiyo bila kupata ushindi.

Yanga itacheza tena na Medeama, Desemba 20 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, katika mechi ya raundi ya nne ya ligi hiyo na baada ya hapo itabakisha michezo miwili, dhidi ya CR Belouizdad kwa Mkapa Februari 23 mwakani na kumaliza na Al Ahly Machi 1 mwakani nchini Misri.

## Simba, Wydad mechi ya hesabu

**Na Saada Akida**

USHINDI ni kauli ambayo inazungumzwa na Simba kuelekea mchezo wa tatu wa Kundi B katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Wydad Casablanca utakaochezwa leo kuanzia saa 4.00 usiku kwenye Uwanja wa Marrakech, nchini Morocco.

Timu hizo zinakutana mara ya tano na katika michezo mitatu Simba ikiwa nyumbani ilifanikiwa kupata ushindi wakati Wydad Casablanca wakishinda mara mbili kwenye Uwanja wa Mohammed V, Morocco.

Ili kufufua matumaini ya kutinga hatua ya robo fainali, Simba inahitaji kuondoka na alama tatu au angalau sare nyingine ya tatu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Simba, Abdelhak Benchikha, alisema amekiandaa vyema kikosi chake kuhakikisha kinarejea Tanzania na pointi tatu muhimu.

Benchikha alisema anafahamu wapinzani wao wanakikosi kizuri na watahitaji kushinda wakiwa nyumbani wakati pia anaamini wachezaji wake watapambana katika mchezo huo ili kupata matokeo chanya.

"Tutafanya kila tunachoweza kuhakikisha tunapata pointi tatu, wachezaji wapo tayari kwa mchezo huu, haitakuwa rahisi kushinda lakini ndio matokeo tunayohitaji," alisema Benchikha.

Kocha huyo alisema Simba itacheza kwa utulivu mechi hiyo ambayo anajua wazi itakuwa ushindani kwa sababu kila upande unataka kupata matokeo mazuri na kujiimarisha katika msimamo wa Kundi B.

Amewataka mashabiki kuungana na timu yao katika maombi ili kufikia malengo ya kuvuna matokeo chanya ugenini ili yawaweke katika njia ya mafanikio kwenye michuano hiyo.

Naye kiungo, Fabrice Ngoma, alisema anawaamini wachezaji wenzake watapambana kuhakikisha wanapata ushindi katika mchezo huo.

"Tutapambana kuhakikisha tunapata pointi tatu, Waarabu wanaushirikiano mzuri na ndio maana wanapata matokeo, hivyo na sisi tutashirikiana, tutapambana kufikia malengo yetu," alisema Ngoma ambaye aliwahi kucheza soka Morocco kwa muda wa miaka mitatu akiwa na Raja Casablanca.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >